Al-Islam.org
Ahlul Bayt Digital Islamic Library Project
Published on *Books on Islam and Muslims | Al-Islam.org* (https://www.al-islam.org)



# Dalili za Qiyama na Ubashiri wa Kudhihiri Imam Mahdi (a)

### Author(s):

Amiraly M. H. Datoo [3]

Kitabu hii ni Dalili za Qiyama na Ubashiri wa Kudhihiri Imam Mahdi (a)

### Category:

Imam al-Mahdi [4]

### Topic Tags:

Qiyama [5]
Wanazuoni [6]
Hadithi [7]

### Person Tags:

Imam al-Mahdi (as) [8]
Imam Ali (as) [9]
Imam Jaffar Sadiq (as) [10]

# Kujitolea

Safina ya msafara wa mwisho wa mwanadamu inakaribia mwisho wake katika dimbwi la hatari ya imani potofu ya kuamini dunia hii tu bila ya kujali Aakhera. Uroho huu umeongezeka katika udanganyifu wetu wa kisayansi kiasi kwamba mwanadamu anataka kuiendesha sayari ya Venus, Mwezi na Jua. Uroho huu umemfanya kiasi cha kuweza kusahau matatizo ya dunia yetu hii.

Mashabiki wa utamaduni wameudhalilisha ubinadamu kufikia tabaka la chini kabisa la aibu kiasi kwamba hata kilio cha Baba Adam a.s. pia kitakuwa kimelowana kwa jasho la udhalilisho.

Kidhahiri, dunia hii imejaa mwangaza lakini kiza cha ujahiliya kinaenea mbali na kwa mapana. Kizazi cha Shetani kimekwisha tayarisha mipango kamambe ya kulipiza kisasi chake cha kudharauliwa na kizazi cha Mtume Adam a.s. Hali mbaya na machafuko ya matendo ya aina yote ya madhambi ndivyo vilivyosababisha kufungwa milango ya mwanadamu ya kuwa huru. Kivuli cha kiza kikubwa cha misiba ndiyo mambo yanayotia uchungu wa moyo juu ya ubinadamu.

"Lakini, mwale wa nuru moja tu wa matumaini katika janga hili la kutokuwa na matumaini ni ile *nuru ya nafsi* yako (Imam MahdiError: Reference source not found a.s. ) ambayo ipo inang'ara mbali na pazia isiyoonekana. Tunakuomba Ewe Imam Mahdi a.s. ! Udhihiri haraka iwezekanavyo na kwamba ufupishe hayo masaa ya subira yetu kwa ajili yako ingawaje kamwe hatuwezi kupoteza subira zetu kwa ajili yako. "

"Tuombee, udhihirishe yale yaliyo batini na uifanye nuru yako ing'arishe ulimwengu mzima. Dhihirisha maneno ya Allah swt kuwa "***Allah swt ataikamilisha nuru yake hata kama makafiri watachukia***". Udhahiri wako ndio dalili ya kuja kwa Siku ya Qayama lakini kutokuwapo kwako pia ni yenye maumivu kama Siku ya Mwisho. Wanaadamu tunaoathirika tunakuhitaji mno na mimi ninayo imani kamili ya kuja kwako na mwelekeo mwema katika kudhihiri na njia moja ya kukukaribisha, kwa kunyenyekea ninakitoa kitabu hiki "***Qayamat-i-Sughra***" mbele yako na natumaini kuwa utanikubalia mimi kama mtumwa wako na hakika hii itakuwa ndiyo uokovu wangu".

Amiraly M. H. Datoo
Bukoba, 4 Januari 1996

# Utangulizi

***Qayamat -i- Sughra*** ni kitabu ambacho kinazungumzia mambo mengi hasa kuhusiana na **ubashiri wa kuja kwa Imam MahdiError: Reference source not found a.s.** , jambo ambalo linakubaliwa na

Waislamu wa Madhehebu zote kwa pamoja kuanzia mwanzoni hadi siku hii ya leo. Waandishi wa Kishiah wamefanya kazi kubwa mno katika swala hili na vile vile juhudi za waandishi wa Kisunni pia zinastahili pongezi kwani wao wamechangia kwa kiasi kikubwa katika kuthibitisha waziwazi kuja kwa Imam Mahdi a.s. .

Hivyo hapa chini munaletewa marejeo ya maandiko kutoka vitabu vya Kisunni:

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | ***Jame' Sahih*** | Muhammad ibn Ismail Bukhari | *Ahadith* 13 |
| 2. | ***Jame' Sahih*** | Muslim ibn Hajjaj. | *Ahadith* 11 |
| 3. | ***Jame' Sahihain*** | Hamidi | *Ahadith* 2 |
| 4. | ***Jama bain Sihah Sitta*** | Zaid ibn Muawiya Abdari | *Ahadith* 11 |
| 5 | ***Fadhail-us-Sahaba*** | Abdul Aziz Abkari | *Ahadith* 7 |
| 6. | ***Tafsir*** | Tha'labi | *Ahadith* 5 |
| 7. | ***Gharib-ul-Hadith*** | Ibn Qataiba | *Ahadith* 6 |
| 8 | ***Al-Firdous*** | Ibn Shirwiyah Dailami | *Ahadith* 4 |
| 9. | ***Musnad-i-Fatimah*** | Hafidh Abul Hasan Darqutni | *Ahadith* 6 |
| 10 | ***Musnad-i-Ali*** | Hafidh Abul Hasan Darqutni | *Ahadith* 3 |
| 11 | ***Al-Mubtada*** | KIssai | *Ahadith* 3 |
| 12 | ***Al-Masabih*** | Husain ibn Masud Atra | *Ahadith* 5 |
| 13 | ***Al-Malahim*** | Abul Hasan Manadiri | *Ahadith* 34 |
| 14 | ***Kitab Hafidh Ibn Mutayyan*** | | *Ahadith* 3 |
| 15 | ***Ar-Riaya-li-Ahlir Riwaya*** | Muhammad Ismail Farghani | *Ahadith* 3 |
| 16 | ***Khabar-i-Soteh*** | Hamidi | *Ahadith* 2 |
| 17 | ***Istiab*** | Yusuf ibn Abdul Aziz Numairi | *Ahadith* 2 |

Katika karne hizi kumi na tatu kumeweza kutokea watu wachache ambao wanakanusha kabisa swala hili la kuwapo kwa Imam MahdiError: Reference source not found a.s. na idadi yao ni ndogo mno. Hapana shaka kuwa kuna watu ambao wanadai kuwa Yazid bin Muawiya bin Abi Sufiyan kuwa khalifa halali. Kunaweza kuwapo sababu mbili tu za kukanusha kuwapo kwa Imam Mahdi a.s. Moja, iwapo wao watakubali na kuthibitisha kuwapo kwa Imam Mahdi a.s. , basi kutakuwa na shauku kubwa ya kutaka kujua shakhsiyah yake na nasaba yake, maisha na mienendo yake, n. k. hivyo mambo yote kama hayo yangalijitokeza mbele yao ambavyo wao wasingaliweza kufanya hila za kuzikubalia taarifa hizo.

Sababu ya pili ni kwamba kumewahi kutokezea watu waongo na ambao walijiita MahdiError: Reference source not found, hivyo watu walikwisha choshwa na wazushi hao kiasi kwamba hawataki kumkubalia Mahdi a.s. wa kweli. Na hii ni mbinu ya kukwepa tu ambavyo hoja kama hizi hazikubaliki katika Islam.

Kwa hakika sisi hatuwajali wale wote wanaomkanusha MahdiError: Reference source not found a.s. kwa hoja zao zisizo na misingi wala faida. Lau hoja zao zingalikuwa halisi na za kimsingi basi kusingalikuwapo na Mahdi wazushi na wafuasi wao. Hapa sisi tunazingatia wale ambao wamejivika Umahdi katika miili yao isiyo toharifu. Kumekuwapo na Mahdi katika Banu Abbas, Banu Fatima,n. k. vile vile mabara yote ya Indo-Pak na Afrika imeshirikiana katika kupatikana kwao. Lakini historia imewakanyaga Mahdi wengi waongo na wazushi.

Tabia na desturi ya mwanadamu imekuwa daima ikivutiwa na mitindo na mambo mapya, vivyo hivyo ndivyo hao MahdiError: Reference source not found waongo ndivyo walivyoweza kufaidi na kuwavutia watu. Imesemekana kuwa wale wotakaomkimbilia Mahdi kwa pupa bila ya kuwa na maarifa kamili, basi wamepotoka – Halakal Mustaji'un!

Kwa hakika zipo Ahadith nyingi mno zilizo sahihi na kutegemewa kuhusu Imam MahdiError: Reference source not found a.s. na hivyo hakuna mwanya wowote ule wa kutokezea Mahdi waongo. Lakini hao wazushi huwa watu wenye hila ambazo wao hujihusisha na ubashiri fulani na huweza kujitangaza kuwa wao ni Mahdi. Kwa bahati mbaya, wale wote wenye elimu ndogo wamekuwa daima wakiwakubali Mahdi kama hao na wakiwazunguka hadi kufa kwa Mahdi mzushi. Hivyo itakuwa ni vyema kwa kuchapisha habari kamili kuhusu Mahdi wa kweli ili mwanya wowote wa upotofu ufungwe kabisa. Faida ya pili ya uchapishaji kama huo utasaidia kuwapambanua Mahdi wazushi bila hata ya kutokezea magomvi na mafarakano.

Kwa mfano, kumekuwapo na kikundi kimoja ambacho kimedai kuwa Mtume Issa a.s. na Imam MahdiError: Reference source not found a.s. ni mtu mmoja tu. Katika swala hili, iwapo mtu atakuwa akijua kuhusu ubashiri wa kuja kwa Imam Mahdi a.s. na kwamba Mtume Issa a.s. atamsaidia na atasali nyuma yake, basi swala hili litajitatua lenyewe bila ya kuzusha ubishi wowote. Vile vile itakuwa vyema iwapo tutajihusisha zaidi katika swala hili. Kuna hoja mbili katika wazo hili:

1. *Masiha* aliyeahidiwa hatakuwa Mahdi bali atakuwa akilingana naye

2. Ipo Hadith moja isemayo kuwa *'La Mahdi illa Masih'* yaani hakutakuwapo na Mahdi illa ni Masihi.

Inawezekana kuthibitisha habari yoyote kama ni kweli kwa kutoa maelezo ya kimantiki. Popote pale panapozungumziwa ubashiri wa Mtume Issa a.s. katika Hadith, basi tujue waziwazi kuwa yeye atakuwa Issa bin Maryam na wala si mtu mwingine kama yeye. Na wala haipatikani Hadith kama hiyo katika maandishi ya Mashia.

Hadith kama hizo zinapatikana katika maandishi ya Masunni ambapo Wanazuoni wao wamezipuuzia na kusema kuwa walioziripoti ni watu dhaifu. Kinyume na hivyo, zipo Hadith nyingi mno ambazo zinaelezea na kuthibitisha kuwa Mtume Issa a.s. atakuwa Mwisraili na MahdiError: Reference source not found a.s. atatokana na kizazi cha Mtume Muhammad s.a.w.w Hivyo imetuwia dhahiri kuwa Mahdi na Masihi ni watu wawili walio tofauti kabisa.

Hao MahdiError: Reference source not found waongo wameleta hasara kubwa miongoni mwa jamii zetu na hivyo halitakuwa jambo la ajabu iwapo Mahdi a.s. wa kweli atapata upinzani. Hivyo inatulazimu kuwa na elimu kamili ya Mahdi a.s. wa kweli. Kwa hakika ulimwengu kwa hivi sasa umejaa matatizo na misiba, na hivyo kumjua mtetezi wetu moyoni mwetu ni jambo la kutufariji mno. Kitabu hiki ni kiungo kimoja cha elimu juu ya Imam Mahdi a.s.

Maandiko ya Mashia yamejaa kwa Ahadith kuhusu Imam MahdiError: Reference source not found a.s.

na kijitabu hiki sio cha kwanza kwa aina yake bali kina habari ambazo zitatuongoza kwa njia haki. Vile vile jambo la kututia moyo ni kwamba habari nyingi mno zimetolewa na Ahli Bayti a.s. ya Mtume s.a.w.w ambapo haziwezi kuwa ni habari za uzushi. Wanazuoni wa Kisunni wamethibitisha usahihi wa Ahadith hizo na wamekana wale wote ambao wanajaribu kupotosha ukweli na usahihi wa Ahadith na riwaya hizo.

Si kazi ngumu kukusanya Ahadith bali kazi iliyo ngumu kabisa ni ile ya kuthibitisha usahihi na ukweli wake hivyo ni vyema kuwadokezea mambo machache kuhusu hayo:

1. Maandiko mengi ya watu wa mji wa *KufaError: Reference source not found* yamepitia mabadiliko kabla ya kutufikia sisi. Wao wamekuwa na utaratibu tofauti wa maandiko yao na katika kuleta mabadiliko ya maandishi,kumeweza kutofautiana katika maana na maelezo. Mfano 'maberamu ***yatachomwa motoError: Reference source not found*** katika mitaa ya Kufa' au inapatikana hivi 'maberamu ***yatachanwa*** katika mitaa ya Kufa'. Mfano wa pili, ipo Hadith inayomzungumzia Auf-Salmi, ambaye makazi yake yanajulikana kama ni Tikrit na kwa mujibu wa maandiko ya Kufa inawezekana pia kupatikana kuwa ni Kuit. Miji yote hiyo miwili ipo Saudi Arabia na ni vigumu kuamua uhakiki wake. Kwa kuchukulia mojawapo ni lazima lakini uasili wa Maandiko ya Kufa yatapotea.

2. Katika riwaya na mapokezi, majina ya miji na mahala pengine yanatumika majina ya kale ambayo kwa sasa hayatumiki tena. Hivyo ni vyema kupata majina yanayotumika kwa sasa sambamba na majina ya kale ili Hadih hizo zieleweke vyema.

3. Taarifa kamili ya kimsingi ya Hadith itolewe, nani aliyeiripoti, mbele ya nani iliripotiwa, mahala pa kuripotiwa, n. k. , ili taarifa hizo ziweze kutambulisha vyema kuhusu Hadith hiyo.

4. Ahli Bayt a.s. ya Mtume Mtukufu s.a.w.w wamerekebisha kipindi katika nyanja mbalimbali za jamii ,maadili, kiuchumi, n. k. Hivyo Ahadith zinazozungumzia mambo ya ubashiri hayatakuwa na mushkeli kueleweka na kukubalika. Vile vile kuna mambo mengine manne pia, nayo ni:

a. Uhakiki,

b. Isiyo na uhakiki

c. Makhsusi,

d. Kawaida.

Ubashiri wowote ule ambao ni wenye uhakiki, basi hayo yatatokea tu katika hali yoyote ile. Na Mabashiri yale yasiyo na uhakiki yanaweza kutokea, inategemea. Mabashiri ya kawaida yanaweza kupatikana kila mahala. Na mabashiri makhsusi yamefungamanishwa na muda na mahala maalum. Ni matumaini kuwa mafungu haya ya uchambuzi yatasaidia kutambua matatizo na mabishano yoyote yatakayotokea.

5. Ahadith za ubashiri hazihitaji tafsiri au maelezo. Ama hayo yamekwishatokea au yatatokea kama vile

yalivyoelezwa. Kwa watu kujaribu kuchambua kwa kuongezea chumvi na pilipili kutaongezea kuleta hali ngumu ya kueleweka na kufahamika.

Ninayo furaha kuwaelezea kuwa kitabu hiki cha ***Qayamat-i-Sughra*** kimejaribu kutimiza mahitaji na masharti kama hayo. Ni jambo la kuvutia kuona kuwa ***Qayamt-i-Sughra*** kinazungumzia mabashiri ambayo hayajatokea bado mfano uasi utakaoongozwa na Hasan Sayyed, Uchokozi wa SufianiError: Reference source not found, kuteketezwa kwa baadhi ya sehemu za Mashariki ya Kati ,n. k. mabashiri ambayo bado Mahdi wazushi hawajaweza kuzibashiri.

Kwa kumalizia mazungumzo haya, ninawaomba wasomaji wote wakisome kitabu hiki kwa makini sana na wala si kwa kuupoteza muda tu bali waweze kuzingatia makusudio ya kuandika kitabu hiki. Imethibitika kwa mamlaka ya QuranError: Reference source not found Tukufu na vile vile Ahadith kuwa ni lazima kuwepo na kiongozi wa Kidini katika ulimwengu na kwamba *mtu yeyote yule atakayekufa bila ya kumjua Imam wa zama zake basi atakufa kifo cha ujahili*. Hivyo elimu na maarifa ya Imam ni swala la Aakhera pia na ambapo ni faradhi kwa wanawake na wanaume wote kwa pamoja.

Mwishoni mwa kitabu hiki nimejaribu kuongezea makala juu ya ***uthibitisho wa kuwapo kwa Imam MahdiError: Reference source not found a.s. kwa mujibu wa Wanazuoni wa Ahli Sunna*** ili msomaji aweze kutambua umuhimu wa Imam Mahdi a.s. katika madhehebu mengine ya Islam.

Amiraly M. H. Datoo
Bukoba, 5 Januari 1996

# Maneno Machache

Kwa jina la Allah swt.

Watu walio hodari humu duniani wanakubali kuwa akili/busara ni mwongozo na mtoa ushauri wa mwanadamu. Huwa inamwongoza kuelekea mema na kumzuia na mabaya. Ni busara hiyo ambayo ndiyo inayomtofautisha mtu na mnyama na kumfanya awe kiumbe bora kuliko wote.

Allah swt anawaamrisha watu watumie busara katika kutatua matatizo yao. Allah swt anatuambia katika Qurani Tukufu kuwa '*aya zake kwa ajili ya wale wanaofikiri*. ' Maneno machache kiasi gani lakini hayakosi hekima ndani yake. Iwapo tutafuata mambo kama vipofu basi hatutakuwa na tofauti na wanyama na labda tutakuwa dhalili kuliko hao kwa sababu mtu kama huyo inavyoonekana hajijali.

Busara bila ya elimu pia ni bure kwa sababu elimu ni nuru ya busara. Lakini elimu ni kiasi kidogo sana kwa kulinganisha na ukubwa wa ulimwengu. Allah swt anatuambia kuwa hatukupewa isipokuwa elimu kidogo tu, rejea ***17:85.*** Hivyo ni ujahili mtupu iwapo sisi tutajigamba kwa elimu yetu kwa kutaka

kukanusha sharia za Allah swt ambapo jambo la msingi ni kutokuelewa kwetu vyema masuala hayo.

Hivyo ni dhahiri kuwa yale yote ambayo yameelezwa na kubashiriwa katia Kitabu cha asili na kudura na yale ambayo yamesemwa na Mtume Mtukufu s.a.w.w hayawezi kamwe kuwa uongo ati kwa sababu sisi hatuelewi. Kila mmoja atakubaliana nasi iwapo tutasema kuwa kazi za kubuni na kufikiri hazina uhakika wowote mbele ya uchunguzi na matendo.

Kujitumbukiza katika mambo ya kubuni na uzushi ni tabia ya Shaitani kwani yeye alijitakabarisha kiasi cha kumuasi Allah swt. Kufuata elimu kwa njia sahihi ni kule kufanya uchunguzi na utafiti juu yake kabla ya kutekeleza. Mtume Muhammad s.a.w.w alisema kuwa "***Mimi ni mji wa elimu na Ali ni mlango wake***" na vile vile alisema kuwa "***Mimi ni hazina ya elimu na Ali ni ufunguo wake***". Kwa hivyo tumepata ushahidi wa Mtume Mtukufu s.a.w.w kuwa kuna shakhsiya waliobarikiwa elimu kwa kudura za Allah swt. Hivyo elimu yake Imam Ali a.s. haiwezi kupimika au kuelezeka.

Kwa hivyo ni faradhi kwetu sote kuamini na kusadiki yale yaliyoelezwa katika Qurani Tukufu na marejeo ya Qurani katika Ahadith za Mtume Mtukufu s.a.w.w na Mrithi wake Imam Ali a.s. na Ahali yake a.s. Haitupasi sisi kamwe kuzikataa semi zao ambazo sisi hatuzielewi kikamilifu. Kutoamini na kutosadiki huku katika Islam kunamfanya mtu akufuru.

Na mojawapo ya maudhui hayo ni kuhusu *QayamaError: Reference source not found* – ambayo ni mojawapo ya misingi ya *Dini* ya Islam. Hivyo kuna mabashiri mengi kabla ya kufikia Qayamah. Mambo yaliyobashiriwa yanapatikana katika QuranError: Reference source not found Tukufu na katika Ahadith. ***Katika mabashiri yote hayo kuna ubashiri mmoja muhimu kabisa wa kuja kwa Imam MahdiError: Reference source not found a.s.*** Na ubashiri huu upo unapatikana katika Aya za Qurani Tukufu, Ahadith, misemo ya Wanazuoni wakuu na Mafuqahaa. Hivyo litakuwa ni jambo la kuaibisha iwapo atatokezea mtu kupinga ubashiri huo ati kwa sababu ya ujahili wake. Jee huyo mtu ataweza kukabiliana na Qurani, Ahadith na wanazuoni?

Waislamu wote kwa ujumla wanaamini kudhihiri kwa Imam MahdiError: Reference source not found a.s. ingawaje kuna tofauti kidogo. Mashiah wanaamini kuwa Imam Mahdi a.s. yu hai na yupo ***ghaibu*** (mafichoni) kama vile walivyo Mtume Issa a.s. , Ilyas, Khizr n. k. Kwa upande wa Masunni wao wanaamini kuwa yeye bado hajazaliwa na atajidhihirisha atakapofikia umri wa miaka arobaini. Kwa mukhtasari, Masunni wanaamini kuwa atakuwa ***ghaibu*** kwa kipindi cha miaka arobaini ambapo wanazuoni wakubwa wanaungana na Mashiah katika masuala hayo.

***Kukanusha kuwapo kwa MahdiError: Reference source not found ni uthibitisho wa kufr, kwa sababu Mtume s.a.w.w amesema kuwa yeyote atakaye kataa kuwapo kwa Mahdi basi ni Kafiri.*** Jambo dogo kabisa linalo tuhakikishia kuwapo kwa Mahdi a.s. ni kule kutokezea kwa Mahdi-bandia ambao wapo wanapatikana katika historia. Kwa hivyo iwapo utataka nakala basi itatokana na nakala asilia, kama hakuna nakala asilia basi huwezi kupata nakala yake. Vile vile kuna habari kamili katika vitabu vya kale kuhusu Imam Mahdi a.s. , nasaba yake n. k. hivyo inatuwia rahisi kwetu sisi kuweza

kutofautisha baina ya Mahid wa kweli na wale bandia. .

Hao MahdiError: Reference source not found bandia wameweza daima kuwazuzua wale wote waliokuwa majahili na wasio zijua sifa za Imam a.s. na ambao hawajui kuhusu ubashiri wa kuja kwa Imam Mahdi a.s. Hivyo ni faradhi kwetu sote kufahamu na kujua elimu na maarifa ya Imam a.s. hasa katika kipindi hiki kilichojaa kwa uovu na dhuluma za kila aina za Shaitani. Watu wengi hawana mapenzi na Dini, na hapa ndipo Shaitani anapopata nguvu na wafuasi wake katika mambo ya maasi. Dunia yetu inakaribia kuangamia kwani dalili za Qayama zipo mbele yetu hivyo kunakaribia kudhihiri kwa Imam Mahdi a.s.

Nimejaribu kuzikusanya mabashiri yote ya kuja kwa Imam Mahdi a.s. ambayo bado hayajatokea katika kitabu hiki na kukipa jina la ***Qayamat-i-Sughra*** ambapo ni matumaini yangu kuwa wasomaji wote watafaidika na kuifanya imani yetu kuwa madhubuti katika Dini na kujitayarisha kumpokea na kukutana na Imam Mahdi a.s. ***Mwokozi na mkombozi wetu sote !***

Sababu ya kukipa jina hili la ***Qayamat-i-Sughra*** ni kwamba Imam MahdiError: Reference source not found a.s. hatadhihiri hadi hapo dunia nzima ichafuke kwa maonevu na dhuluma kwa kiasi cha kupindukia. Hivyo jina hili linamaanisha ***'kipindi kitakachotangulia QayamaError: Reference source not found'***

Kitabu hiki kimezungumzia na kugusia mambo mengi mno zikiwemo itikadi za watu, dini zao, mila na desturi, utamaduni, elimu,mawazo na fikara zao. Hivyo ninawaombeni nyote kunitumia maoni yenu kwa kukubalia maandiko au kuyapinga au kuyafafanua zaidi ili yanisaidie katika kuendeleza kazi hii iwe vyema zaidi hapo siku za mbeleni. Yote mutakayonitumia lazima ziwe na hoja na ufafanuzi mzuri kwani zitaweza kuingizwa katika chapa zitakazokuja.

*Hatimaye ninatoa shukrani zangu za dhati kwa wote.*

5 Januay 1996
Amiraly M. H. Datoo
P. O. Box 838,
Bukoba, Tanzania (E. Africa)

# Qayamat Au Siku Ya Hukumu

Nguzo ya tano katika Dini ya Islam ni kuamini katika *QayamaError: Reference source not found*. Na imani katika nguzo hii ni faradhi kwani ni siku moja maalum iliyokwisha pangwa, na swala la lini ni siri ya Allah swt na Waja wake makhsusi. Zipo mabashiri mengi yatakayotokezea kabla ya kuja kwa

*QayamaError: Reference source not found*. .

Mtume Mtukufu s.a.w.w ameripotiwa kusema: "Zipo dalili kumi kutokezea kabla ya kuja kwa *QayamaError: Reference source not found*:

1. Uasi wa *SufianiError: Reference source not found*.

2. Kuja kwa *DajjalError: Reference source not found*

3. *MotoError: Reference source not found na moshi*

4. *Dabbatul Ardh*

5. **Kudhihiri kwa Imam MahdiError: Reference source not found a.s**.

6. *Kuchomoza kwa jua kutoka Magharibi*

7. *Kuja kwa Mtume Issa a.s. kutokea mbinguni*

8. *Kuachinika kwa ardhi katika Mashariki*

9. *Kuachanika kwa ardhi katika Bara la Arabia*

10. *Moto Error: Reference source not foundundani mwa AdenError: Reference source not found ambayo itawakusanyisha watu katika ardhi tambarare*. 1

---

1. Katika maneno ya Mtume Mtukufu s.a.w.w tumepatiwa ishara tu. Moto na moshi vinaweza kumaanisha mabomu ambayo yanapolipuka hutoa moto na moshi. Moto undani mwa Aden unaweza kusemwa kuwa moto katika matanki ya kuhifadhia mafuta ya petroli au visima vya mafuta vya Arabia. Tabaka za chini ya ardhi za Arabia yamejaa kwa mafuta.

# Ubashiri Wa Kuja Kwa Imam Mahdi A.S.

Wale waliokuwa wakitoa ubashiri walikuwa wakiishi huko *Bara la Arabia* na walikuwa wakijua vyema kiwango fahamu za watu wenzao na hivyo tutaona kuwa ubashiri mwingi utazungumzia Mashariki ya Kati. Popote pale walipokuwa wakiulizwa maswali, wao walikuwa wakizingatia elimu na fahamu ya mwulizaji. Zipo jumla zingine zilizotumika kijumla kama 'ardhi' n. k. katika mabashiri.

Jambo lingine la kukumbuka ni kwamba kumetokea mabadiliko na hata kamili katika mazingira na kisiasa kuanzia wakati huo. Majina ya miji imebadilika na miji mingi kuangamizwa kabisa na ikatoweka. Na miji mipya kutokezea. Hivyo ni ombi kwa msomaji kujaribu kupitia vitabu vya jiografia vya mambo ya

kale ili aweze kupata ufafanuzi zaidi.

Ilikuwa ni desturi ya Waarabu kujulikana kwa majina ya baba, familia au ukoo, hivyo ndivyo ilivyo tumika muundo huo huo katika majina humu kitabuni.

Ubashiri wa kuja kwa Imam MahdiError: Reference source not found a.s. umegawanywa na kuchambuliwa kama ifuatavyo:
(1) Ubashiri wa kawaida,
(2) Ubashiri maalum na
(3) Ubashiri wa lazima.

## (1). Ubashiri wa Kawaida.

Abdullah ibn Abbas (r. a. ) amesema kuwa baada ya kumaliza *Hajj* ya mwisho (mwaka wa 10 Hijriyyah), Mtume Mtukufu s.a.w.w alisimama mbele ya mlango wa Ka'aba Tukufu, akiwa ameshikilia komeo ya mlango, huku akiwauliza ma-Sahaba wake: ***"Je, nikuambieni dalili za siku ya QayamaError: Reference source not found?"*** Salman Farsi (r. a. ) ambaye alikuwa karibu naye,alisema: "Ndiyo, Ewe Mtume wa Allah swt. "

Mtume Mtukufu s.a.w.w akasema, "Hakika, miongoni mwa dalili za *saa*, ni kuwa:
(1) watu watapuuza salaError: Reference source not found,

(2) watafuata matamanio yao wenyewe

(3) wataelekeza kujipendelea wao wenyewe,watawaheshimu matajiri

(4) na watauza Dini yao kwa manufaa ya kidunia

(5) wakati huo roho na moyo wa Muumin itayayuka (kwa huzuni) kama chumvi inavyoyayuka katika maji,kwa sababu ataona mambo yaliyoharamishwa na hataweza kuyabadili. "

Salman akasema: "Haya yatatokea,ewe Mtume wa Allah swt?"
Mtume Mtukufu s.a.w.w akasema: "Ndiyo,naapa kwa Aliyonayo roho yangu mkononi mwake. "

"Ewe Salman,:
(6) wakati huo watawala watakuwa wadhalimu

(7) Mawaziri watakuwa waasi,

(8) na wadhamini (wale waliopewa amana kwa kuaminiwa) watafanya hiana

(9) hakika wakati huo maovu yatakuwa mema na mema yatakuwa maovu

(10) wale wafanyao hiana wataaminiwa na waaminifu watafikiriwa kuwa si waaminifu;

(11) na mwongo atasadikiwa,na msema kweli atahesabiwa mwongo

(12) Wakati huo kutakuwapo na utawala wa wanawakeError: Reference source not found

(13) Masuria watashauriwa

(14) na watoto watakaa juu ya mimbarError: Reference source not found

(15) udanganyifu utahesabiwa kuwa ni uerevu

(16) na Zaka itakuwa ni kama kutozwa faini;

(17) na mateka ya vita (yaani mali ya ummahError: Reference source not found) yatakuwa kama ni mali ya mtu binafsi;

(18) na mtu atakuwa mjeuri kwa wazazi wake na atakuwa mwema kwa marafiki zake

(19) na wakati huo kutatokea na nyotaError: Reference source not found zenye mikia (comets). "

Salman akasema: "Haya yatatokea, ewe Mtume wa Allah swt?"

Mtume Mtukufu s.a.w.w akasema: "Ndiyo, naapa kwa Aliyonayo roho yangu mkononi mwake. "

"Ewe Salman!:
(20) wakati huo mwanamke atakuwa mshiriki wa mumewe katika biashara,

(21) na mvuaError: Reference source not found itakuwa motoError: Reference source not found sana

(22) na watu wema watabaki katika huzuni;

(23) na masikini hawata heshimiwa;

(24) na wakati huo masoko yatakaribiana,

(25) Tena huyu atasema,"Mimi sikuuza chochote, na yule atasema, "Mimi sikupata faida yoyote. " Kwa hivyo hutamkuta mtu yeyote asiyemlalamikia Allah swt.

"Ewe Salman!
(26) tena itatokea iwapo watu watawazungumzia watawala wao, watawaua, na ikiwa watanyamaza kimya, watanyang'anywa mali yao, watanyimwa heshima zao, watamwaga damuError: Reference source not found yao na mioyo ya watu itajaa woga; kisha hutamwona mtu yeyote ila atakuwa mwoga, mwenye khofu, ametishika na ameshstushwa”

"Ewe Salman!
(27) Bila shaka wakati huo mambo fulani yataletwa kutoka Mashariki

(28) na mambo fulani yataletwa kutoka Magharibi,

(29) Basi ole kwa watu walio dhaifu (wa imani) katika UmmahError: Reference source not found wangu kutokana na hayo; Ole ya Allah swt iwe kwa hayo. Wao hawatakuwa na huruma juu ya wadogo wao, wala hawatamsamehe yeyote aliyefanya kosa. Miili yao itakuwa ya wanadamu, lakini mioyo yao itakuwa ya mashetani. "

"Ewe Salman!
(30) Wakati huo wanaumeError: Reference source not found watawaashiki wanaume,

(31) na wanawakeError: Reference source not found watawaashiki wanawake;

(32) na watoto wa kiume watapambwa kama wanawake;

(33) na wanaume watajifanya kama wanawake

(34) na wanawake wataonekana kama wanaume;

(35) na wanawake watapanda mapando (farasi na ngamia)

(36) Hapo tena patakuwepo laana ya Allah swt juu ya wanawake wa UmmahError: Reference source not found wangu. "

"Ewe Salman!
(37) Bila shaka wakati huo MisikitiError: Reference source not found itapambwa (kwa dhahabu n. k. ) kama inavyofanywa katika masinagogi na makanisa,

(38) na *QuranError: Reference source not found* zitapambwa (kwa nakshi na rangi za kupendeza n. k. )

(39) na minara ( ya misikiti) itakuwa mirefu; na safu za watu wanaosimama katika salaError: Reference source not found zitazidi, lakini nyoyo zao zitachukiana na maneno yao yatatofautiana. "

"Ewe Salman!
(40) Wakati huo wanaumeError: Reference source not found watatumia mapambo ya dhahabu; kisha watavaa hariri,n a watatumia ngozi za chui. "

"Ewe Salman!
(41) Wakati huo ribaError: Reference source not found itakuwako,

(42) na watu watafanyia biashara kwa kusemana na rushwa

(43) na dini itawekwa chini, na dunia itanyanyuliwa juu. "

"Ewe Salman!
(44) Wakati huo *talaqaError: Reference source not found* zitazidi

(45) na Sheria ya Allah swt haitasimamishwa. Lakini hayo hayatamdhuru Allah swt. "

"Ewe Salman!
(46) Wakati huo watatokea wanawakeError: Reference source not found waimbaji,

(47) na ala za muziki

(48) na wabaya kabisa watawatawala UmmahError: Reference source not found wangu. "

"Ewe Salman!
(49) Wakati huo matajiri katika UmmahError: Reference source not found wangu watakwenda Kuhiji kwa matembezi, na walio wastani kwa biashara,na masikini kwa kujionyesha.

(50) Hivyo basi wakati huo watakuwapo watu ambao watajifundisha *QuranError: Reference source not found* si kwa ajili ya Allah swt na wataifanya *QuranError: Reference source not found* kama ala ya muziki.

(51) Na watakuwapo watu ambao watasoma dini si kwa ajili ya Allah swt

(52) na idadi ya wanaharamu itazidi

(53) watu wataiimba *QuranError: Reference source not found*,

(54) na watu watavamiana kwa uroho wa kidunia. "

"Ewe Salman!
(55) Haya yatatokea wakati heshima zitakapoondoka, na madhambi yatatendwa

(56) na watu waovu watakuwa na uwezo juu ya watu wema,

(57) na uongo utaenea na mabishano (matusiError: Reference source not found) yatatokea

(58) na umasikini utaenea,

(59) na watu watajivuna kwa mavazi yao

(60) na itakuwepo mvuaError: Reference source not found wakati si wake

(61) na watu watacheza dama, kamari na Ala za muziki,

(62) na hawatapenda kuhimizana mema wala kukatazana maovu

(63) na kwa ajili hali itakavyokuwa hata itafikia wakati huo kuwa Muumin atakuwa na heshima ndogo kuliko hata mjakazi

(64) na wanaosoma na wanaotumia wakati wao katika kumwabudu Allah swt watalaumiana.

(65) Hao ndio watu watakaoitwa wachafu na wanajisi katika Ufalme wa mbinguni. "

"Ewe Salman!
(66) Wakati huo matajiri hawataogopa chochote isipokuwa mtu masikini; hadi kwamba masikini wataendelea kuomba kati ya ijumaa mbili, na hawatamwona mtu yeyote wa kutia chochote mikononi mwao. "

"Ewe Salman!
(67) Wakati huo itazungumzwa *Ruwaibidhah. "*

Salman akauliza: "Ni nini *Ruwaibidhah* ? Ewe Mtume wa Allah swt, baba na mama yangu wawe fidia kwako. "

Mtukufu Mtume s.a.w.w akajibu:
(68) "Watu fulani watazungumza kuhusu mambo ya watu ambayo hayakuwahi kuzungumzwa namna hii zamani.

(69) Tena baada ya muda mchache machafuko yatatokea duniani,na kila nchi itafikiri kuwa machafuko yapo katika nchi yao tu. "

(70) "Watabaki katika hali hiyo kwa muda ambao Allah swt atapenda wabaki;

(71) kisha ardhi itatapika vipande vya moyo wake dhahabu, fedha na madini mengineyo;

(Hapo Mtume s.a.w.w ) alinyosha kidole chake penye nguzo, na akasema: "Kama hizi (kwa ukubwa), lakini siku hiyo dhahabu wala fedha hazitamsaidia mtu yeyote. Na hii ndiyo maana ya maneno ya Allah swt ***'Hakika dalili Zake zimekuja. '***[1]

Zipo habari zingine zilizoelezwa katika vitabu vinginevyo kwa kupitia Jabir Ibn Abdullah Ansari, ambavyo ninazitaja:

"Ewe Salman! Wakati huo:
(1) Wazee watajitumbukiza katika mambo ya ushirikina na uchawi,

(2) *ghiba* ndiyo itakuwa mazungumzo yenye kupendeza,

(3) mali iliyopatikana kwa njia za haramu, itachukuliwa kama ndiyo neema,

(4) wazee hawatakuwa na mapenzi ya wadogo na vile vile wadogo hawatawajali wazee na kuwaheshimu

(5) Islam itabakia kwa jina tu kwani wafuasi wake hawatakuwa wakifuata maadili na maamrisho yake,

(6) Kimbunga kikubwa cha rangi nyekundu kitatokezea mbinguni na kutaanguka mawe kutoka mbinguni

(7) nyuso zitakuwa za kuchukiza

(8) kutakuwa na mitetemeko na kuporomoka kwa ardhi kila mara.

Hapo Sahaba walimwuliza Mtume s.a.w.w , "Ewe Mtume wa Allah swt, je lini yatakapotokea hayo yote?" (pamoja na nishani na dalili za hapo juu, baadhi zimeongezeka hapa chini)

Mtume s.a.w.w aliwajibu:
(9) Watu watakuwa watumwa wa *shahwa* au matamanio yao

(10) watu watakuwa walevi wa kupindukia kwani matumizi ya uleviError: Reference source not found utakithiri na utakuwa ukipatikana kwa udhahiri bila ya watu kuona aibu ya aina yoyote,

(11) Wanaume watakuwa wakiwatii wake zao,

(12) jirani atakuwa wakiwaudhi na kuwatesa majirani wenzake,

(13) Wakubwa hawatakuwa watu wenye huruma, mioyo yao itakuwa imejaa kwa maonevu,

(14) vijana hawatakuwa na heshima

(15) watu watajenga majumba imara na marefu mno,

(16) wafanyakazi watadhulumiwa hakiError: Reference source not found zao,

(17) ushahidi wa kiuongo utachukuliwa kuwa wa kawaida,

(18) ndugu atakuwa akimwonea wivu ndugu yake halisi

(19) watu watakaokuwa wakifanya biashara kwa ushirika, basi watakuwa daima wakifikiriana mbinu za kumdhulumu mwenzake,

(20) mambo ya zinaaError: Reference source not found yatakuwa kama kawaida kwani yatatendeka na kusikika pia.

(21) ile mioyo ya kutaka kusaidia watu wengine itakuwa imetoweka,

(22) Maasi na dhuluma itaongezeka kupita kiasi,

(23) matumbo ya watu itachukuliwa kuwa ndiyo miungu yao, kwani hawatajali kiwevyo, ilimradi wapate chochote kile,

(24) wanawakeError: Reference source not found watakuwa wakitawala akili za wanaumeError: Reference source not found na watakuwa wakiwaendesha wanaume vile watakavyo wao,

(25) kutatokea Maulamaa au wanazuoni waovu kabisa kwani watajionyesha kuwa ni wacha Mungu na

wenye elimu, ambapo kwa hakika watakuwa waroho wa mali ya dunia tu. "

Hapo Mtume Mtukufu s.a.w.w aliwaonya: "Kumbukeni, wakati kama huo utakapokuja, basi Allah swt atatumbukiza watu katika balaaError: Reference source not found za aina nne:
(1) kutawaliwa na watawala dhalimu
(2) ukame na vitu vya matumizi ya kila siku kuwa bei ghali yaani kupanda kwa maisha,
(3) dhuluma za watawala
(4) kuabudu miungu. "

Sahaba waliposikia hayo walishtushwa na kuuliza: "Ewe Mtume wa Allah swt ! ***Je kweli kuwa Mwislamu atakuwa akiabudu miungu na masanamu?"***

Mtume s.a.w.w aliwajibu: "Naam! Kwao mapesa yatakuwa kama miungu kwani watakuwa wakiziabudu kupindukia kiasi. "

Kwa hakika sisi tunayashuhudia haya yote yakitokea ambayo Mtume s.a.w.w amekwisha bashiri karibu karne kumi na nne zilizokwishapita. Imam Ali a.s. katika khutba yake ijulikanayo kama *Al-Bayan* anaelezea ubashiri kwa undani zaidi. Wasomaji wenye kutaka kupata habari zaidi wanaweza kutazama (1) *Yanabi-ul-Muwaddah* (2) *Basharat-ul-Islam,* Sayyid Mustafa Ali-Sayyid Haider al-Kazami, chapa ya BaghdadError: Reference source not found.

## Ubashiri ya Imam Ja'far As-Sadiq A.S.

Mazungumzo yafuatayo yamefanywa na Imam Jaafer as-Sadiq a.s. ambamo ameripoti ubashiri wa siku za mwisho wa dunia hii. Yametolewa kutoka *Darul Islam, Bihar-ul-Anwar* na *Raudhat-ul-Kafi.* Wanaoripoti habari hizo ni Allamah Naraqi na Sheikh Kulaini r. a. kutokea kwa Himran.

Imam a.s. alisema:
(1) "Haki itakuwa imetokomezwa na watu walio katika hakiError: Reference source not found hawatapatikana.
(2) Dhulma na uonevu utaenea katika miji yote.
(3) Kufuata *QuranError: Reference source not found* kimatendo itajulikana kama tabia ya kizamani.
(4) Zitatolewa maana ya Aya za *QuranError: Reference source not found* kwa mujibu wa matakwa ya watu, hivyo mafhum ya *Quran* itakuwa imebadilishwa na kupotoshwa.
(5) Wadhalimu watakuwa wakiwa kandamiza wale walio katika haki.
(6) Uchokozi na uchochezi utatokea kutoka kila pande na pembe.
(7) Matendo maovu na kukosa aibu vitaenea na kuzagaa kila mahala.
(8) UlawitiError: Reference source not found utakuwa ni jambo la kawaida.
(9) Muumin atakuwa akionekana kama mtu dhalili ilhali waovu watakuwa wakiheshimiwa
(10) Vijana hawatakuwa wakiwaheshimu wakubwa wao
(11) Huruma itakuwa imepotea kabisa.

(12) Waovu watakuwa wakitukuzwa kwa udhalimu wao na hakutakuwapo na mtu yeyote wa kuwapinga.
(13) Wanaume watafurahishwa mno kwa kuingiliana na wanaumeError: Reference source not found wenzao.
(14) Wanawake watawaoa wanawakeError: Reference source not found wenzao.
(15) Mapesa yatatumika kwa ajili ya matumizi yale yaliyo haramishwa na Allah swt.
(16) Starehe, anasa na zinaaError: Reference source not found zitashamiri.
(17) *ZinaaError: Reference source not found* itajulikana kama maadili yaliyopitwa na muda.
(18) Muumin atatengwa kwa sababu ya kufanya ibada za Allah swt.
(19) Jirani mmoja atafurahi mno kwa kumuudhi na kumbughudhi jirani mwenzake.
(20) Wazushi (kama Salman Rushdie wa Uingereza) watatukuzwa na kusifiwa katika kueneza fitina na yale wanayozusha.
(21) Ushauri mzuri utakanwa.
(22) Milango ya wema yatafungwa wakati milango ya maovu yatafunguliwa.
(23) *Al-KaabaError: Reference source not found* haitatumika au haitafikika kwa sababu ya vikwazo na ugumu utakaowekewa mahujaji.
(24) Watu watalazimishwa kuacha kwenda *MakkahError: Reference source not found* kuhiji.
(25) Watu hawatakuwa wakitimiza ahadi zao watakazokuwa wakizitoa.
(26) Wanaume watakuwa wakitumia dawa za kuamsha tamaa za kiume kwa ajili kulawiti na wanawakeError: Reference source not found watakuwa wakitumia vyakula vya mafuta ili kujitayarisha kwayo.
(27) Baadhi ya wanaume watakuwa wakiishi kwa kujipatia mapesa kwa kuuza mikundu yao
(28 ) na wanawake watakuwa wakijipatia mapesa kwa kufanyisha biashara uuke wao.
(29) Wanawake watаunda vilabu vyao, mashirika na umoja wao.
(30) Wanaume atajigeuza kama wanawake na watavutia na wanawake.
(31) Wanaume watajirembesha kama wanawake.
(32) Ulawiti utachukuliwa kama ndiyo ustaarabu na starehe ya kweli. Na Banu Abbas watalipia ulawiti.
(33) Wanawake wataona fakhari kwa kuwa na waume nje ya mume mmoja wa ndoa na vivyo hivyo wanaumeError: Reference source not found watakuwa hivyo hivyo.
(34) Heshima itakuwa ikitolewa kwa utajiri wa mtu na wala si ucha Mungu.
(35) ribaError: Reference source not found ndiyo itakayokuwa biashara ya kila siku.
(36) Ushahidi wa uongo utakuwa ukisadikiwa mno.
(37) Kile alichokiharamisha Allah swt kitachukuliwa ni halali na chochote kile alichokihalalisha Allah swt kitachukuliwa ni haramu.
(38) Maamrisho ya Dini yatageuzwa kwa mujibu wa matakwa yao.
(39) Wachokozi na waovu watatenda maovu kwa udhahiri bila ya khofu yoyote ile na Muumin hawataweza kuwazuia vyovyote vile.
(40) Watawala watawapenda mno Makafiri kuliko Muumiin.
(41) RushwaError: Reference source not found ndiyo itakuwa njia ya kujitimizia kazi kutoka maofIssa wanaohusika.

(42) Wanaume wata walawiti wake zao.
(43) Watu watakuwa wakiuawa kwa visingizio vidogo vidogo na magomvi madogo madogo.
(44) Wanawake watawafanyia wanaume dhihaka, nao watashawishiwa kufanya uhusiano na wanawakeError: Reference source not found.
(45) Wanaume wataishi kwa mapato ya wake zao zitakazopatikana kwa zinaaError: Reference source not found.
(46) Wanawake watakuwa wakiendesha hukumu majumbani huku wanaume wakiwatii wake zao kwa sababu wanawake hao ndio watakuwa wenye mapato.
(47) Wanawake watatumiwa katika kupatikana huduma mbalimbali.
(48) Kula kiapo kwa jina la Allah swt litakuwa ni jambo lililowekwa ulimini.
(49) PombeError: Reference source not found na kamari vitapatikana kila mahala na vitakuwa vimezagaa.
(50) wanawakeError: Reference source not found wa Kiislamu wataingiliana na Makafiri, ambapo Waislamu hawataweza kuwazuia na wala hawatakuwa na uwezo kama huo.
(51) Maadui wetu watasaidiwa na watawala na marafiki zetu watadhalilishwa kiasi kwamba hata kiapo chao hakitakubaliwa.
(52) Udanganyifu na hila ndizo zitakuwa desturi miongoni mwa watu.
(53) Usomaji na usikilizaji wa *QuranError: Reference source not found* utakuwa ni bughudha kwa watu.
(54) Kusikiliza mambo fidhuli ndiyo itakuwa ikipendelewa na watu.
(55) Jirani hatamstahi jirani mwenzake illa kwa khofu ya ulimi mkali na mchafu.
(56) Sheria na kanuni za Allah swt hazitatambuliwa na waovu hawataadhibiwa kwa maamrisho hayo.
(57) *Ghiba* na kulaghaiana ndivyo vitakuwa vitu vya kawaida.
(58) Madhumuni ya *Hajj* na *Jihad* yatakuwa mbali na yale ya Kiislamu.
(59) MisikitiError: Reference source not found itarembeshwa kwa dhahabu.
(60) Watawala watawataka ushauri kwa nia ya Makafiri.
(61) Litakuwa ni jambo la kawaida kuibia katika uzani na vipimo vya biashara.
(62) Kumwaga damuError: Reference source not found ya watu wegine litakuwa ni jambo la kawaida.
(63) Watu watajigamba kwa ndimi zao chafu zenye matusiError: Reference source not found mabaya ili kuwatishia watu wengine.

Imam a.s. aliendelea kusema:
(64) "Watu watakuwa wakipuuzia salaError: Reference source not found na kutojali.
(65) Watu hawatakuwa wakilipa *zakaError: Reference source not found* ingawaje watakuwa na utajiri mkubwa.
(66) Sanda za maiti zitakuwa zikiibiwa na kuuzwa tena
(67) Mauaji yatakithiri mno kiasi kwamba hata wanyama pia wataanza kuuana wenyewe kwa wenyewe.
(68) Watu watakuwa wakisali katika mavazi ya kiajabu.
(69) Macho na mioyo itapoteza nuru zao za heshima na huruma.
(70) Watu watakuwa wamejishughulisha na maswala ya kutafuta mali na mapesa tu.

(71) Watu watasali kwa kuonyesha tu.

(72) Watu watatafuta elimu ya Dini kwa ajili ya kujipatia mali ya dunia.

(73) Ushirika katika makundi yatakuwa ndiyo mambo ya maisha.

(74) Wale watakaojipatia riziki kwa njia ya halali, watasifiwa kwa midomo tu.

(75) Matendo maovu na machafu yataenea hata *MakkahError: Reference source not found* na MadinaError: Reference source not found.

(76) Watu waliokufa watafanyiwa mizaha na vichekesho.

(77) Mwaka hadi mwaka hali itakuwa ikiendelea kuharibika kuwa mbaya zaidi.

(78) Matajiri wataigwa.

(79) Masikini, mafukara watafanyiwa dhihaka na kufedheheshwa.

(80) Matukio ya kudura kama yale ya mitetemeko, maporomoko n. k. yatakuwapo lakini watu watakuwa hawaviogopi.

(81) Matendo maovu yatakuwa yakitendwa kiwaziwazi.

(82) Wazazi watatupa watoto wao na watoto watawatusi wazazi wao na daima watakuwa wakitaka mali na utajiri wa wazazi wao.

(83) Wanawake hawatawatii na kuwafuata waumeError: Reference source not found wao.

(84) Siku itakayopita bila ya mtu kutenda madhambi, basi itachukuliwa ni siku yenye nuksi.

(85) Watu wenye uwezo wataficha mali muhimu na kuviuza kwa bei ya ulanguzi.

(86) Waombaji na walaghai watajumuika katika kucheza kamari na kulewa.

(87) PombeError: Reference source not found itatumika kama ni kitu chenye kuponya yaani dawa.

(88) Makafiri watatukuzwa juu ya watu wengine na Muumin watadhalilishwa na kupuuzwa.

(89) Kutafanywa malipo kwa ajili ya kutoa Adhan na salaError: Reference source not found.

(90) MisikitiError: Reference source not found itajaa kwa watu wasiokuwa na khofu ya Allah swt.

(91) Watu wenye fahamu na akili kasoro ndio watakaokuwa wakiongoza *salaError: Reference source not found za jamaa'* na watu kama hao kamwe hawatashutumiwa au kusutwa na badili yake wataheshimiwa. "

## (2) Ubashiri Maalum

Mtume Mtukufu s.a.w.w amesema: "Kabla ya kuja kwa QayamaError: Reference source not found, vitu vitatu vitakuwa vya kawaida

(1) ugonjwa wa bawasiri,

(2) vifoError: Reference source not found vya ghafla,

(3) Saratani ya damuError: Reference source not found.

Vile vile Mtukufu Mtume s.a.w.w amesema: "Mojawapo ya sharti kwa kuja Siku ya *QayamaError: Reference source not found* ni motoError: Reference source not found utakaotanda Mashariki hadi Magharibi. "

Ameendelea kusema, "Idadi ya wanawakeError: Reference source not found itazidi idadi ya

wanaumeError: Reference source not found kwa uwiano wa wanawake hamsini kwa mwanamme mmoja. "

## Kuangamizwa Kwa Nchi Na Miji Mbalimbali

Mwanachuoni mkuu wa Kisunni Mohiuddin, ameandika katika *Muhadherat-ul-Abrar* na *Muthammerat-ul-Akhyar,* riwaya kutoka Ilyas, mtiririko hadi kumalizikia kwa Hudhaifah, kuwa Mtume Mtukufu s.a.w.w alisema:
1. "MisriError: Reference source not found haitaangamizwa hadi hapo BasraError: Reference source not found imeteketezwa, Basra itateketezwa kwa sababu ya IraqError: Reference source not found na Misri itaangamizwa kwa sababu ya mto Nile.

2. *MakkahError: Reference source not found* itatekwa na Ethiopia.

3. MadinaError: Reference source not found itakumbwa na mafuriko.

4. YemenError: Reference source not found itateketezwa na ndui.

5. Eila itaangamizwa kabisa katika kutekwa.

6. Uajemi utatekwa na Saalik kutoka Dailam na Dailam atatimuliwa na Waarmenia na wao watatekwa na WaturukiError: Reference source not found.

7. Waturuki watakumbwa na kuangamizwa kwa radi.

8. Sind itatolewa na IndiaError: Reference source not found

9. na India itapinduliwa na Wachina.

10. Error: Reference source not foundChinaError: Reference source not found itaharibiwa na mchanga au nzigeError: Reference source not found.

11. Rafdha itaipoteza Ethiopia.

12. *SufianiError: Reference source not found* atawatilia vikwazo wale wanaokwenda kuzuru makaburi ya Mtume Mtukufu s.a.w.w na Maimamu a.s.

13. Ramla itateketezwa nusu na

14. Iraq itakumbwa na ukame.

## Mitume Sitini Bandia

Abdullah ibn Umar anaripoti kuwa Mtume Mtukufu s.a.w.w alisema: "QayamaError: Reference source not found haitakuja hadi MahdiError: Reference source not found atakapodhihiri kutokana na kizazi

changu; na yeye pia hatajitambulisha hadi hapo patakapotokea watu sitini watakaodai kuwa wao ni mitume (bandia). "

## Vita Pamoja Na Weupe Na Maangamizo

Imeripotiwa katika kitabu cha *Aqdud Dur* cha Auf Ibn Malik kuwa mimi nilimwijia Mtume s.a.w.w ambapo alipokuwa ameketi katia hema lenye rangi ya udongo. Kwa utaratibu alitawadha na kuniambia, "*QayamaError: Reference source not found* inasubiri ubashiri sita:
(1)mvuaError: Reference source not found ya changarawe kutoka mbinguni (labda inaweza kumaanisha kuporomoka kwa mabomuError: Reference source not found na matokeo yake). Hili ndilo la kwanza. "

Mimi nilimjibu: "Naam, Bwana wangu!"

Aliendelea Mtume Mtukufu s.a.w.w:
(2) "Ushindi wa kuishinda *JerusalemError: Reference source not found*.
(3) Mauaji kupindukia kiasi. Watu watakuwa wakiuawa kama ng'ombe na mbuzi.
(4) Kuzidi kwa mali ambayo haitoshelezi kukamilisha matakwa ya mtu.
(5) Yatatokea magomvi na hakuna hata nyumba moja itakayobakia salama bila ya kukumbwa na magomvi hayo.
(6) Watu weupe watawageuka. Wao watakushambulieni katika mabatalioni themanini na kila batalioni litakuwa na askari kumi na mbili elfu.

## Kuteketezwa kwa Baadhi ya Miji

Katika *Manaqib* ya Ibn Shahar Ashub imerekodiwa kutoka kwa Qatada ambaye ameripoti kutoka Saeed Ibn Musayyab: "Imam Ali a.s. aliulizwa juu ya Aya ya *QuranError: Reference source not found* Tukufu: *Na hakuna taifa lolote ila alipita humo Muonyaji.'* Hapo Imam Ali a.s. alitoa tafsiri ndefu mno na humo alitoa ubashiri wa kuangamizwa kwa baadhi ya miji.
1. *Samarqand, Jaj, Khwazim*, *Isfehan* na *KufaError: Reference source not found* vitaharibiwa na WaturukiError: Reference source not found. (Hapa Waturuki wanamaanishwa WarusiError: Reference source not found) .

2. *Hamadan* na *Ray* yataangamizwa na watu wa Kazvin.

3. *Tabrusa, MadinaError: Reference source not found* na sehemu ya Ghuba ya Uajemi yatakumbwa na ukame na njaa.

4. *MakkahError: Reference source not found* itatekwa na Ethopia.

5. *BasraError: Reference source not found* na *Balkh* yatazama majini.

6. Sind itatwaliwa na India.

7. Error: Reference source not foundIndia na Tibet

8. Tibet na ChinaError: Reference source not found.

9. Majeshi yatatetemesha *Badakshan, Saani Kirman* na baadhi ya sehemu za SyriaError: Reference source not found.

10. YemenError: Reference source not found itaangamizwa na watawala

11. *Sijistan* na baadhi ya sehemu za Syria zitaangamizwa kwa gesi

12. *Saman* itaangamizwa na magonjwa na nzigeError: Reference source not found wataiharibu *Marv*

13. Nyoka watua viumbe katika *Hirat*

14. *Naishapur* itateketezwa.

15. *Azarbaijan* itavamiwa na majeshi na radi kali zitapiga (labda kwa sababu ya mabomuError: Reference source not found)

16. Mto *Nile* utafurika

17. *Bokhara* itazama majini

18. Kutakuwapo na ukame na miji ya *Salam* na *BaghdadError: Reference source not found* itaangamizwa.

## Ubashiri wa Ziada wa Imam Ali A. S.

Abu Abdullah Jafar ibn Muhammad anaripoti kutoka kwa Imam Husain a.s. ambaye alimwuliza baba yake: "Tafadhali sana baba naomba utuambie ni lini Allah s.w.t. ataitakasa ardhi kutokana na watu waovu?"

Imam Ali a.s. alimjibu: "Ardhi haitaweza kamwe kutakasika hadi hapo damuError: Reference source not found ya wazushi itakapokuwa imekwisha mwagika kikamilifu. "
Watoto na wanawake watakuwa watawala.

(47). Taratibu za tawala za nchi
Taratibu za tawala za nchi zitakuwa zikipata sura mpya mpya za kutawala vile vile utawala wa kifalme utatokomea.

(48). Kizingiti baina ya ardhi na mbingu

Kutaonekana kitu kama kizingiti baina ya ardhi na mbingu, kweli litakuwa ni jambo la kustaajabisha kabisa hasa Mashariki ya Kati.

(49). Jumuiya ya wale wasio waumini

Jumuiya ya wale wasio waumini wataenea Bara la Arabia na nchi nyingine za Kiarabu (ama wao ni WarusiError: Reference source not found au WachinaError: Reference source not found kwani Warusi wameishajidhatiti katika nchi nyingi za Kiarabu).

(50). Kuwasili kwa WachinaError: Reference source not found

Kuwasili kwa WachinaError: Reference source not found katika Bara la Arabia ni ubashiri mkubwa wa vita vikubwa hali mbaya kabisa isiyoelezeka itatokea baada ya wao kuwasili huko.

(51). Michafuko ya kila aina

Kutakuwa na michafuko ya aina mbalimbali kuanzia Azarbaijan na Armenia. Machafuko haya yataenea hadi mlima mwekundu. Matokeo haya na hatima yake yatakuwa mabaya kiasi kwamba watoto watakuwa kama wamezeeka na wazee watatamani mauti. Machafuko haya yatafika mpaka mji wa KufaError: Reference source not found kupitia Wast na vita hatari kabisa vitatokea karibu na mji wa Najaf. Kwa hakika maovu na matisho haya hayaelezeki. Vile vile vita vitatokezea karibu na Teheran.

(52). Kuzuia kizazi

Kutakuwa na mipango mbalimbali ya kuzuia kizazi na mbinu hizo zitashurutishwa kwa njia mbalimbali.

---

1. Habari hizi tazama Day of Judgement ,Sayyid Saeed Akhtar Rizvi,Bilal Muslim Mission of Tanzani,DSM,chapa ya pili,1978,uk. 44. ,naye amenakili kutoka Bihar-ul- Anwar,j. III.
2. Kwa msomaji atakayependa kufanya utafiti zaidi juu ya swala hili juu ya Ubashiri,anaweza kusoma Hotuba ya Imam Ali a.s. Al-Makhzun katika kitabu kiitwacho Basharatul-Islam,chapa ya Baghdad.
3. Leo duniani tunaona kuwa maendeleo ya sayansi yametudhihirishia kuwa kuna uwezekano wa kufikisha Sauti na sura duniani kote hasa kwa kupitia satellites. Sasa jee kuna ugumu gani kwake Allah swt kufanya kudra zake?
4. Mambo kama haya ndivyo yanavyotokea katika kupiga kura za kidemokrasia!
5. Kwa utumwa hapa kunamaanisha mbinu za kumfanya mtu asiweze kusema dhidi ya mambo ya mfadhili wake kama vile tunavyoona na kusikia kuhusu masharti ya misaada itolewayo na nchi na watu wafadhili.
6. Nimesikia katika Idhaa ya Kiswahili ya BBC mnamo tarehe 17 Novemba 1995 saa 6. 30 jioni kuwa Chuo Kikuu cha Al-Azhar University cha huko Misri kimetoa fatwa kuwa mwanamme anaweza kujigeuza k,uwa mwanamke na vile vile mwanamke anaweza kugeuzwa kuwa mwanamme kwa njia za operesheni ati kwa sababu ni maumbile yake ndivyo yalivyo.

   Vile vile nimesikia katika idhaa ya Kiingereza ya BBC hivi majuzi (wiki moja kabla ya Fatwa kutoka Al-Azhar) kuwa kumefanywa uchunguzi na utafiti huko Amerika na kutolewa ripoti kuwa mtu khanisi na anayelawiti na kulawitiwa aachwe awe hivyo na wala asilaumiwe na jamii kwa sababu ndivyo yalivyo maumbile yake.
7. Tunajionea vile nchi za Kiarabu zinavyopingana na kupigana wenyewe kwa wenyewe kwa ajili ya ushawishi wa nchi za Magharibi. Utengano miongoni mwao unatokana na kulaghaiwa na nchi za Magharibi ambavyo ni vyema kwa maslahi yao.

# Udondozi Kutoka Vitabu Vya Kiarabu

Ingawaje mabashiri yote yaliyoelezwa katika kurasa zilizopita yametoka katika vitabu vingi vya Kiarabu mabashiri yafuatayo yanatoka khususan kutoka kitabu kimoja kiitwacho *al-malahim wal fitan.* Bashiri hizi zilikusanywa na bwana mmoja anayejulikana kwa jina la Ali ibn Musa ibn Jaafer ibn Muhammad ibn Taus Ali Hasan wal-Husaini. Kitabu hiki kilisambazwa kwa mara ya kwanza katika mwaka wa 604 A. H. Taasisi inayojulikana kwa jina la *Manshuratul Atba'atul Haidariyyah* huko mjini Najaf. Mabashiri haya yalikusanywa zaidi ya karne saba zilizopita:

(**1**). Mtume Mtukufu s.a.w.w amesema: "Jihadharini na benderaError: Reference source not found nyeusi mwanzoni mwake ni mbaya katikati mwake kuna upotofu na mwishoni wake ni ukafiri (utawala huo unagawanywa katika sehemu tatu kipindi cha kwanza, kipindi cha pili na kipindi cha mwisho ).

(**2**). Mtume Mtukufu s.a.w.w amesema: "Mjikusanye mnapoona benderaError: Reference source not found nyeusi msiendeshe mikono yenu na mikuki yenu muisimamishe kutatokezea watu warefu na jumuia isiyoaminika isiyotegemewa itatokezea, mioyo yao itakuwa migumu kama chuma wao watakuwa matajiri lakini watasita kutimiza wajibu wao, wao watawaita watu katika mambo mema lakini wao wenyewe watakuwa wamepotoka majina yao yataanza katika majina ya urithi (ukoo) hoja zao na busara zao zitafanana na zile za wanawakeError: Reference source not found, kutaongezeka kutokezea kwa ikhtilafu baina yao na hatimaye Allah swt atawabainishia ukweli.

(**3**). Mtume Mtukufu s.a.w.w ameshauri: "Kimbieni kwa usalama wenu pale mtakapoona benderaError: Reference source not found za rangi nyekundu zikipepea huko MisriError: Reference source not found. Watakapofika SyriaError: Reference source not found, lazima muanze kutenda matendo. Kimbieni hata kama mtaweza kufika mbinguni kimbieni juu ya mawingu kama mtaweza ama sivyo mjaribu kujihifadhi mahali popote duniani. Hadithi ya juu hiyo ilinakiliwa na Hasan.

(**4**). Msimulizi anasema: "Nilimsikia Abdullah ibn Omar akisema akiwa katika Ka'abaError: Reference source not found kutatokezea benderaError: Reference source not found nyeusi kutoka Mashariki na bendera za rangi ya njano kutokea upande wa Magharibi, watawala wa bendera zote hizo mbili watapambana vikali huko SyriaError: Reference source not found kwa hakika ni maafaError: Reference source not found na maangamizo makubwa kabisa (kwa kuwa msemaji alikuwa akiongelea katika Kaaba hivyo upande wake wa Mashariki ni Iran na upande wake wa Magharibi ni MisriError: Reference source not found. ).

(**5**). Hasan Basir ameripotiwa akisema "kutokea ndani mwa Teheran kutatokezea mtu mmoja atainuka, ataitwa jina la Shuayb ibn Saleh Tamimi, mtu huyo atakuwa rangi nyeupe, kifua kipana na ndevu zilizochakaa. Mtu huyo atakuwa akiwaongoza watu elfu nne wenye benderaError: Reference source not found rangi nyeusi atakuwa na bendera ya Imam MahdiError: Reference source not found a.s. ambavyo atakuwa hawezekani katika vita.

(**6**). Muhammad Hanafi anaripotiwa kwa kusema mwanzoni benderaError: Reference source not found nyeusi itakuwa ya Bani Abass na baadaye zitatokezea Khorasan. Kofia zao zitakuwa nyeusi na nguo zitakuwa nyeupe au inaweza kumaanisha upande wa juu wa bendera unawezekana ukawa mweusi na

upande wa chini ukawa mweupe, kiongozi wa kikundi hicho atakuwa Shuayb ibn Saleh Tamim. Wao watawashinda wenyeji wa Sufiani na watafika hadi mji wa Jerusalem na baada ya kufika Jerusalem watamkabidhi Imam MahdiError: Reference source not found a.s. mamlaka yote na vile vile watamsaidia. Kiasi cha watu mia tatu wa SyriaError: Reference source not found watamsaidia Shuayb ibn Saleh Tamim ibn Saleh. Kitakuwa ni kipindi cha miezi sabini na miwili baina ya kuinuka kwa Shuayb na kudhihiri kwa Imam Mahdi a.s.

(**7**). Makhul anaripoti kuwa Mtume Mtukufu s.a.w.w amesema: "Mimi nimeona vyema kutumia jina *Turk* kuliko kutumia neno la WarusiError: Reference source not found. WaturukiError: Reference source not found watakuja mara mbili mara ya kwanza watatokezea upande wa Azarbaijan na mara ya pili majeshi yao yatapitia mto wa Furati (Euphrate) baada ya hapo wataacha mashambulizi yao (Hapa waturuki wanaomaanishwa kutokea upande wa Azarbaijan sio watu wengine bali ni Warusi) .

(**8**). Hodhaifa Yamani ameripoti kuwa Mtume s.a.w.w amesema: "Piganeni kabisa na WaturukiError: Reference source not found mtakapowaona wameingia *Bara la Arabia* Mpigane nao mpaka washindwe ama sivyo wataharibu heshima yenu. Msaada wa Allah swt uwe pamoja nanyi (Ubashiri huu unaelezea uingiliaji wa dola za Magharibi huko *Bara la Arabia* utakuja kutokomezwa ). "

(**9**). Abu Hureira ameripoti kuwa Mtume Mtukufu s.a.w.w amesema: "Kufufuliwa kwa ajili ya siku ya QayamaError: Reference source not found haitatokea hadi hapo kupite vita dhidi ya WaturukiError: Reference source not found. Waturuki hao watakuwa na nyuso nyekundu, macho madogo na pua zilizo pana. Nyuso zao zitakuwa ngumu kama chuma kilichonyooshwa. "

(**10**). Mtume s.a.w.w amesema: "WaturukiError: Reference source not found watasonga mbele haraka haraka wakielekea Tigris. Watakuwa na vyombo vya kusafiria vya rangi ya njano wakijipanga katika mistari kuelekea mto wa Tigris. "

(**11**). Mtume s.a.w.w amesema: "Ninaona kuwa WaturukiError: Reference source not found wanasafiri juu ya mafarasi wenye masikio mafupi, mguu mmoja huku mguu mmoja upande wa pili na wanawafunga mafarasi wao kandoni mwa mto. "

(**12**). Utambulisho zaidi wa WaturukiError: Reference source not found, Mtume s.a.w.w amesema: “Wafuasi wangu itawabidi wapigane vita dhidi ya wale watu wanye nyuso pana, macho madogo na wenye miili migumu. Kutatokezea mashambulizi mara tatu. Safari ya kwanza watu wangu watakimbia ili kujinusurisha kwa mashambulizi, ya pili, baadhi ya watu wangu watauawa na wengine wataponea chupuchupu na katika mashambulizi ya tatu maadui watashinda. Na wao ni Waturuki. Kwa hakika misafara yao itakuwa inawekwa nje na kuzunguka MisikitiError: Reference source not found ya Waislamu. Umma wangu utakuwa katika hali ya hatari. Wao watakuwa wakikimbia, wakichukua kile chochote wapatacho ili waweze kukimbia navyo. "

(**13**). Imam Hasan a. s ameripoti kuwa Mtume s.a.w.w amesema: “Siku ya QayamaError: Reference source not found haitafika kabla ya nyinyi kupambana na watu wafupi na wenye nyuso pana na mashambulio ya pili pamoja na wale watu ambao viatu vyao vitakuwa vimetengenezwa na nywele. Wale watu wa kwanza watakuwa ni WaturukiError: Reference source not found na wale wa pili watakuwa ni wa-Qurdi. "

(14). Kaab ameripoti kuwa Mtume s.a.w.w amesema: "WaturukiError: Reference source not found watakuja katika *Bara la Arabia* Mafarasi wao watakunywa maji ya mto Furati. Hapo Allah swt atawaambukiza ugonjwa mbaya nao watauawa. Hakuna hata mmoja miongoni mwao atakayebaki hai. " Katika hadithi nyingine imeelezwa kuwa WaturukiError: Reference source not found watakuja katika upande wa kushoto wa Mto Tigris. Watakapofika IraqError: Reference source not found wao watakumbana na kuanguka kwa theluji na magonjwa ya kuambu- kizwa hapo, wao watakufa kwa idadi kubwa sana.

(**15**). Kuingia WachinaError: Reference source not foundError: Reference source not found katika *Bara la Arabiia* - Abdullah ibn Omar anaripoti kuwa Mtume s.a.w.w amesema: "Bani Qantura (Wachina) watawadhalilisha watu wa Khurasan na Sijistan. Wao wataendelea na msafara wao hadi watakapofika katika mabustani huko PalestinaError: Reference source not found, hapo baadaye watawaonya watu wa BasraError: Reference source not found waache ardhi zao waondoke. Hapo baadaye wao watajigawanya katika makundi matatu, kundi moja litaelekea Magharibi, kundi la pili litaendelea SyriaError: Reference source not found na kundi la tatu litajihami dhidi ya maadui.

(**16**). *Habari za Bani Qantura*: Abu Hureira anaripoti kuwa washambuliaji watakuwa na macho kama ya mijusi. Nyuso zao zitakuwa na ngozi zilizo ngumu, wao watabainisha vita sehemu tatu: "Kwanza baina ya eneo la mto Furati na mto Tigris. Pili Kijiji cha Mazhar-e-Hamar, kijiji kaskazini mwa SyriaError: Reference source not found, tatu ufukoni mwa mto Tigris wao watadhibiti njia zote zipitiapo hapo na kila atakayekuwa akipita atalazimishwa alipe Dinar mia moja. Na kiwango hicho cha kutoza watu hela za kuvuka zitakuwa zinaongezwa kila mara.

(**17**). Mtume s.a.w.w amesema: "Katika kipindi hicho wenye mabendera makubwa watayachana mabendera madogo, hali hii ya kushambuliana itaendelea hadi hapo kutakapokuja kundi la watu wenye nyuso pana na macho madogo. Watu hao watakuwa ni Bani Qantura (WachinaError: Reference source not found). Wao watapitia Kurdistan huko IraqError: Reference source not found na watawashinda baada ya kuwashambulia Wakurdi, baadaye watawakabili Waarabu na kutatokea vita vikali kabisa ambavyo vitasababisha miji kubakia mitupu, watu wote watakuwa wamekimbia. Hapo baadaye kutatokea mitetemeko na ardhi itapasuka na ardhi nyingi itadidimia watu watakimbia huku na kule bila kujua wanapokwenda. Eneo la kwanza la kuteketezwa litakuwa ni mji BaghdadError: Reference source not found. Kutafuatia na kuvurugika na kuchafuliwa kwa MisriError: Reference source not found. Mutakapoanza kuona hizi bishara zikitokea huko SyriaError: Reference source not found basi muelewe kuwa kuna kifo kila mahala. Hapo ndipo mtaona WazunguError: Reference source not found wanaanza mbinu na hila zao, watakapofika *Bara la Arabia* kutazuka mapambano makubwa ya kuteketeza.

(18). Mtume s.a.w.w amesema: "Utawala wa Waarabu utakwisha". Kauli hii aliitoa mara tatu kiasi kwamba wanaoiripoti walimuuliza, Je ni nani atakayeumaliza utawala wa Waarabu?" Hapo Mtume s.a.w.w alijibu: "(Bani Qantura) jumuia ile ambayo nyuso zao ni pana wana pua tambarare na wana macho madogo. Wao wataingia *Bara la Arabia* kwa sababu vita vikali vitakuwa vimeanza kutokezea. " Hapo WaturukiError: Reference source not found wataleta masharti ya usuluhishi kwamba Waarabu wawarudishie wale wote wasio Waarabu. Waarabu watawaambia wale wasio Waarabu marafiki zao

wajiunge na Waturuki. Hapo marafiki wa Waarabu watawaambia Waarabu, Ole wenu! Kwenu nyinyi kuupa mgongo Uislamu (kwa kuvunja umoja na jumuia yao).
Hapo baadaye marafiki wa Waarabu watapigana peke yao na watawashinda na kuwateketeza maadui zao. Waarabu watakapoona marafiki zao wamenufaika kwa vita wataanza kuomba hisa humo. Hapo marafiki wa Waarabu watasema: "Kwa hakiError: Reference source not found ya Allah swt! Hatutawapeni chochote kwa sababu nyinyi mmevunja uhusiano wetu. "

## Je Waturuki Ni Akina Nani?

Ni udanganyifu kuelewa kuwa wale watu wanaoishi katika nchi ya Uturuki ya leo ndio wanaitwa WaturukiError: Reference source not found. Kwa mujibu wa mwanahistoria Farishta, asili ya Waturuki wanaanzia kwa Mtume Nuh a.s. ambaye alikuwa na mtoto Yafis na huyo alikuwa na mtoto akiitwa Turki. Popote pale kizazi hicho kilipofika waliitwa Waturuki. Mtoto mwingine wa *Yafis* alikuwa akiitwa *Chin*. Ardhi kubwa sana iliitwa kwa jina lake ambayo leo ndiyo ChinaError: Reference source not found. Hivyo katika utafiti huu inatudhihirishia wazi wazi kabisa kuwa Waturuki na WachinaError: Reference source not found ni watu wawili waliotofauti.
Katika jangwa la Gobi kuliishi makabila mawili tofauti, kabila moja lilikuwa likiitwa Mongoli na lingine lilikuwa likiitwa Turuki mababu zao walikuwa sawa. Hao Wamongoli walikuwa wakijulikana kama *Yun*. Na mababu zao walifika hadi katika ya Urusi. Wao walikuwa wakijulikana kwa majina tofauti tofauti kama Yuji, Quishen n. k. WachinaError: Reference source not found waliendelea kuwaita *Yuji*. Kabila zilianza kujulikana kama WaturukiError: Reference source not found katika karne ya sita kizazi kimojawapo kiliishi Azarbaijan katika karne ya tano. Kwa mujibu wa baadhi ya wana historia wao walichukua sehemu muhimu iliyokuwa karibu na Marv hapo baadaye kabila hilo lilitawanyika mbele na kuchukua ardhi ambayo leo inajulikana kama Uturuki. Popote pale walipokwenda wao wanajulikana kama Waturuki na kwa sababu hiyo katika ramani utaona kuna sehemu nyingi zinazoitwa Turkistan ya ChinaError: Reference source not found,Turkastan ya Urusi, n. k. Watu waliokuwa wakiishi katika Turkistani ya China walikuwa na macho rangi ya buluu, nywele nyekundu na warefu. Maumbile haya hayalingani na maumbile na wa-China wa siku hizi.
WaturukiError: Reference source not found ambao waliiteketeza IranError: Reference source not found, IraqError: Reference source not found n. k. walikuwa ni wa-Mongolia. WachinaError: Reference source not found wa siku hizi hawafanani na Waturuki na hivyo wao ndio wanajulikana kama *Bani Qantura* kwa mujibu wa Hadithi. Hivyo Waturuki ambao wanazungumziwa katika Hadithi tukufu za Mtume s.a.w.w ni WarusiError: Reference source not found na *Bani Qantura* ni Wa-ChinaError: Reference source not found na *Bani Asfar* ni WazunguError: Reference source not found.
Tofauti hizi lazima tuzizingatie vizuri na tuzitilie maanani kabisa vivyo hivyo itabidi kuzingatia mipaka ya kijiografia ya ChinaError: Reference source not found ya siku hizi haioani na ile ya zama za Mtume s.a.w.w
Kauli ya Imam Muhammad Baqir a.s. ambayo imetolewa kutoka *Majlis-i-Thannia* ya Sayyid Muhsin Al Amin Al Husein, Al Amir wa Beiruti.

Imam Ali a.s. amesema: "Kutatokea mfarakano mkubwa sana baada ya kufika kwa WarusiError: Reference source not found katika *Bara la Arabia* na WazunguError: Reference source not found kufika katika PalestinaError: Reference source not found na mifarakano hiyo itasababisha kuangamia na kuteketea kwa SyriaError: Reference source not found ambayo itatokea baada ya mapigano baina ya wapinzani wa benderaError: Reference source not found tatu (Bendera tatu inamaanisha kutakuwa na makundi matatu yanayopingana) bendera hizo zitakuwa ni za: (1). Sayyid Hasan, (2). Bani Omaiyya, na (3). Bani Qais.

Mabango ya Sayyid Hasan yatatokezea IranError: Reference source not found, benderaError: Reference source not found ya Bani Omaiyya itatokezea SyriaError: Reference source not found na bendera ya Bani Qais itatokezea MisriError: Reference source not found.

Imam a.s. aliendelea kutoa usia: "Lazima mtulie, msijitie kwenye harakati, mikono yenu na miguu yenu pale mtakapoona dalili hizi, lakini nyinyi hamtawaona (watu wa zama hizo). Dalili hizi ni:
(1) Kuwasili kwa WaturukiError: Reference source not found katika *Bara la Arabia*,
(2) Kuwasili kwa WazunguError: Reference source not found katika PalestinaError: Reference source not found,
(3) Waturuki, WarusiError: Reference source not found, watakaribishwa vizuri kabisa pale watakapofika *Bara la Arabia*.
Hivyo hivyo Wazungu watakaribishwa vyema kabisa na WayahudiError: Reference source not found pale watakapoingia PalestinaError: Reference source not found.

## Mawaidha Ya Mtume S.A.W.W Kuhusu Kujihami

Ibn Masud anaripoti kuwa Mtume s.a.w.w amesema: "Mjikumbatie pale mtakaposikia sauti toka mbinguni katika mwezi wa Ramadhani, kwa sababu kutakuwa na misukosuko mingi katika mwezi wa Shaban. Vita vya wenyewe kwa wenyewe na umwagaji wa damuError: Reference source not found kupindukia kiasi vitaanza katika mwezi wa Dhilqaad, mauaji na uporaji na kila aina ya wizi vitaanza katika mwezi wa dhil-hijjah. Mwezi wa Muharram ni mwezi wa pekee kwa aina yake (kwa huzuni ya Muharramu ndiyo imepita mipaka yake isiyoweza kuelezwa).

Hapo baadaye Mtume s.a.w.w alisema mara tatu: "Loh, loh, loh,! Idadi kubwa kabisa ya watu watauawa wakati huo. "

Mwenye kuripoti alimwuliza Mtume s.a.w.w wakati huo: "Ewe bwana wetu ! Je hiyo sauti ya kutisha toka mbinguni itakuwaje na itatokea lini?"

Mtume s.a.w.w alimjibu: "Sauti hiyo ya kutisha na kushtusha itatokea katika mwezi wa Ramadhani katikati ya siku. Muwe tahadhari kwani sauti hii itamwamsha yeyote atakayekuwa amelala na yeyote yule atakayekuwa amesimama ataketi. Baada ya kumaliza salaError: Reference source not found ya Ijumaa muingie majumbani mwenu mfunge milango yenu yote na kuziba matundu yote yatakayokuwemo

ndani mwa nyumba zenu. Zibeni masikio yenu kwa uangalifu na mzizuie pumzi zenu. Mwangukieni Mola wenu mtakapohisi sauti hiyo na muombe *Subhanal Quddus, Rabunal Quddus*. "Mtu yeyote atakayefanya hivyo ataokoka na mshirikina ataangamizwa. "

Muda huo tarehe, mwezi na siku tunavijua katika Hadith kwa mujibu wa *Hijaz* lakini sisi huku kwetu tuangalie tofauti ya muda ili tujue kwetu hapa itatokea muda gani, vile vile katika baadhi ya Hadith Maimamu a.s. wameripotiwa kusema tarehe 23 mwezi wa Ramadhan. Jambo hili linafanya swala hili liwe wazi zaidi.

Jambo lingine la kuzingatia hapa ni kwamba: Usia huu tumepewa kama tahadhari. Labda inawezekana tunatanabahishwa na mashambulizi ya ndege na kutupwa kwa mabomuError: Reference source not found kunaweza katika zama hizo kukazuka vita vikali, ndege zitaanza kutupa rIssasi ovyo na mabomu ambavyo vitaangamiza watu hivyo watu wanashauriwa kuingia majumbani kujifungia ndani na wamwombe Allah swt awaepushe na balaaError: Reference source not found ipite.

## Kuonekana Mkono Na Uso Mwezini

Imerekodiwa katika *Majlis –i– Thannia* kuwa Moman anaripoti kutoka kwa Imam Jaafer Sadiq a.s. ambaye anasema: “Kabla ya kutokezea sauti kubwa ya mlipuko wa anga kutaonekana dalili tatu katika mbingu. Mwenye kuripoti alimwuliza: "Je ni dalili gani hizo "Imam alimjibu: “Uso wa mwanadamu utaonekana ukinga’a na mkono utaonekana katika mbingu(labda inamaanisha mwanadamu atafika mwezini na katika stesheni zinginezo huko juu).

## Kutokezea kwa SufianiError: Reference source not found: Kuinuka na Kuanguka Kwake.

(1) Hudhaifa Yamani ameripotiwa akisema: “Wa-*SufianiError: Reference source not found* wataingia MisriError: Reference source not found na kuiteka nchi hiyo kwa miezi minne. Atakuwa na utawala wa mauaji na wenye vitisho sana wanawakeError: Reference source not found watalia kwa kupoteza heshima zao, jamaa zao na hadhi zao. Watu watakuwa wakiomba wafe ili wapone na dhuluma watakazokuwa wakifanyiwa".

Katika Hadith nyingine zinaripotiwa kuwa baada ya *SufianiError: Reference source not found* kuiteka MisriError: Reference source not found,*SufianiError: Reference source not found* atatuma jeshi lake kwenda MadinaError: Reference source not found hawa wanajeshi watakuwa waovu kabisa na kupambana na Muslim ibn Akbar baadaye wataelekea *MakkahError: Reference source not found*. Watakapofika Beda wote watakufa kwa kupasuka ardhi na wote watatumbukia katika ardhi na kumezwa.

(2) Imam Muhammad Baqir a.s. amesema: “Uasi wa *SufianiError: Reference source not found* na kudhihiri kwa MahdiError: Reference source not found a.s. vitatokea katika mwaka mmoja.

Katika habari nyingineyo imeripotiwa kuwa *SufianiError: Reference source not found*, Yamani na Khurasani wote watatu watatokezea katika mwaka huo mmoja.

Imam Jaafer Sadiq a.s. amesema: "*SufianiError: Reference source not foundError: Reference source not found* atatokezea katika mwezi wa Rajab na atamiliki Damascus, YemenError: Reference source not found, Jordan, PalestinaError: Reference source not found na Qansain.

Imam Zainul Abedin a.s. amebashiri kabla ya kudhihiri kwa MahdiError: Reference source not found a.s. atatokezea mtu kutoka Kuwait aitwaye Auf Aslami. Huyo atauawa katika Msikiti huko SyriaError: Reference source not found, baada ya hapo Shuayb ibn Saleh atatokezea katika Samarkand na *SufianiError: Reference source not found* atatokezea huko PalestinaError: Reference source not found.

## Moto

(1) Imam Muhammad Baqir a.s. amesema: "Utakapoona motoError: Reference source not found mwekundu njano ukiwaka siku tatu au siku saba mfululizo huko Mashariki basi ujue ndio wakati wa kudhihiri kwa Imam MahdiError: Reference source not found a.s. 1 umefika

(2) MotoError: Reference source not found mkubwa sana utatokezea huko *Bara la Arabia* .

Imam Jaafer Sadiq a.s. vile vile amebashiri kutokezea kwa motoError: Reference source not found katika Mashariki.

## Mtume Issa a.s.

(1) Imerekodiwa na Imam a.s. kuwa Mtume Issa a.s. atateremka *Baitul Muqaddas* wakati wa salaError: Reference source not found ya alfajiri ambapo watu watakuwa wanajitayarisha kusali. Imam MahdiError: Reference source not found a.s. atamkaribisha na kumwambia, karibu, njoo utuongoze katika sala, Mtume Issa a.s. atamchukua Imam mbele na yeye mwenyewe atasali nyuma ya Imam a.s.

(2) *DajjalError: Reference source not found* atakuwa na wanajeshi elfu sabini, Mtume Issa a.s. atakapowaona tu miili yao itakufa ganzi, hali yao ya kupigana vita na Mtume Issa a.s. na Imam MahdiError: Reference source not found a.s. itayeyuka kama vile chumvi inavyoyeyuka katika maji. Mtume Issa a.s. atawateketeza Mayahudi wote na ataivunja misalaba na kuwaua nguruwe.

Hivyo kurudi kwa Mtume Issa a.s. humu duniani kunamaanisha ndiyo mwisho wa dini ya Judea na dini ya Kikristo kwa sababu atakanusha kusulubiwa na kuwapo sharia katika Tawrati inayoharamisha ulaji wa nguruwe. Hivyo tunaweza kuelewa vyema zaidi sababu ya Allah swt kumweka hai Mtume Issa a.s. hadi kudhihiri kwa Imam Mahdi a.s. kwa sababu mtu yeyote anapotaka kukabiliana (kuhusu mazushi) vyema na watu hivyo inambidi yeye mwenye akabiliane nao ndipo litakapokuwa jambo la msingi.

## Nyota Yenye Mkia

Jabir Jaufi anaripoti kutoka Imam Jaafer Sadiq a.s. kuwa: "Wakati khalifa wa Bani Abbas alipozuru Khorasan, nyotaError: Reference source not found yenye mkia ilitokezea ambayo ilikuwa ikiitwa *Al-Qarb-Zushshifa*. Nyota hii ya mkia ilionekana kabla ya kuangamia kwa ukoo wa Mtume Nuh a.s. na wote walizama katika tufani ya maji vile vile nyota hii ilitokezea mbele ya Mtume Ibrahim a.s. na hatimaye yeye akatupwa katika motoError: Reference source not found. Nyota hii ilionekana tena kabla ya kuangamizwa kwa FiraunError: Reference source not found katika zama za Mtume Musa a.s. Nyota hii ilionekana tena wakati Yahya ibn Zakaria (John Babtisti alipouawa). Hivyo mwombeni Allah swt awaokoeni wakati mnapoona hii nyotaError: Reference source not found yenye mkia mbinguni. Kuonekana kwake kutafuatia kwa kupatwa kwa mwezi na kupatwa kwa jua. Baada ya kuonekana kwa nyota yenye mkia kutachomoza benderaError: Reference source not found nyeusi na nyeupe ama bendera ya rangi ya buluu na nyeupe huko MisriError: Reference source not found, na huu ndio mwanzo wa machafuko na majanga na machafuko ya kila aina kutokezea. Nyota hii itaonekana katika mwezi wa *Safar* (mwezi wa pili katika Kalenda ya Kiislamu).

Vile vile imerekodiwa kuonekana kwa nyotaError: Reference source not found yenye mikia miwili huko mbinguni na hii ni ishara katika kipindi kifupi kabla ya kudhihiri kwa Imam MahdiError: Reference source not found a.s. nyota hiyo itaonekana iking'ara kama mwezi.

## Dalili Ziatakazoendelea kwa Miezi Sita

Mtume Mtukufu s.a.w.w. amesema: "Kutaonekana mstari wima wa mwanga baina ya ardhi na mbingu katika mwezi wa Ramadhani. *Shawwal* utakuwa ni mwezi wa machafuko. Kutakuwa na machafuko na magomvi kila mahali katika mwezi wa *Dhil-Qaad*. Misafara ya wale waendao kuhiji itashambuliwa na kuporwa, na barabara ziendazo kuhiji zitawekewa vipingamizi. Haya yote yatatokea katika mwezi wa *Dhil-hijja* wakati mambo ya kutisha mno ya mwezi wa *Muharram* hayawezi kuelezeka.

## Habari Zaidi Kuhusu Syria

(**1**). Abdullah ibn Umar ameripoti kuwa Mtume s.a.w.w amesema: "Mwisho wa dunia utaanza pale kutakapoanza kushtushwa kwa vichwa. Na wakati haya yataanza kutokea, basi ndio mwanzo wa maangamizo ya mwanadamu". Alipoulizwa Mtume Mtukufu s.a.w.w juu ya umuhimu wake, alijibu ndiyo maangamizo ya SyriaError: Reference source not found. Maangamizo na mateketezo hayo yataanzia Syria.

(2). Katika kitabu cha *Al-Malahim wal Fitan* imeandikwa kuwa upotofu utazuka na kutawanyika katika SyriaError: Reference source not found kama vile mchezo wa watoto. Na wala hakuna nyumba yoyote itakayosalimika. Hayo yataendelea mpaka kudhihiri kwa Imam MahdiError: Reference source not found a.s.

## Majanga

Utafika wakati wanaumeError: Reference source not found wataanza kuwauza wakeError: Reference source not found zao ili mradi wapate chakula kidogo. Vile vile utafika wakati ambapo baba atamwuza binti wake mzuri kwa hoja hiyo hiyo.

## Muda wa Utawala wa Imam Mahdi A.S.

Imeripotiwa kuwa Imam MahdiError: Reference source not found a.s. atatokana, atakuwa ndiye Khalifa wa mwisho wa Bani Hashim. Yeye atatawala kwa muda wa miaka arobaini. Yeye ataikomboa Roma na Kostantinopoli.

*Hadith* kama hiyo imeripotiwa na Muhammad Hanafi akiongezea kuwa *JerusalemError: Reference source not found* itajengwa upya wakati wa utawala wake. Mtume Issa a.s. atatokezea baada ya kukombolewa kwa Roma na Kostantinopoli.

## Kuishinda India

Imam MahdiError: Reference source not found a.s. atapeleka batalioni ya jeshi lake moja kutoka *JerusalemError: Reference source not found* kwenda IndiaError: Reference source not found. Jeshi hilo litaishinda India na kuchukua mali ya thamani iliyokuwa imezikwa hadi *JerusalemError: Reference source not found*. Mji huo mtukufu wa *JerusalemError: Reference source not found* utarembeshwa. Jeshi hilo litakuwa na kituo chake hapo IndiaError: Reference source not found hadi kushindwa kwa *DajjalError: Reference source not found*.

## Maafa Yatakayowafikia Waislamu

(**1**). Imerekodiwa kuwa Abdulla ibn Umar amesema: “Umma wa Mtume Muhammad s.a.w.w watakabiliana na maafaError: Reference source not found matano, mawili kati ya hayo yamekwisha kupita na matatu yatatokezea:- (a). matatizo katika Urusi (b). Matatizo yatakayoletwa na WazunguError: Reference source not found (c) matatizo yatakayoletwa na DajjalError: Reference source not found. Baada ya hapo hakutakuwa na matatizo yoyote lakini matatizo haya matatu yatakuwa makali na mabaya kabisa kiasi kwamba watu watahama kutoka nafasi moja kwenda nafasi ya pili kama wanyama na watu watauawa kama ng'ombe na mbuzi wanavyouawa kwa idadi kubwa kabisa.

(**2**). Mtume Mtukufu s.a.w.w amesema: “Umma wangu utafanya maovu yote kama vile mauaji hayo yalivyokuwa yakifanywa na umma wa Mitume iliyotangulia.

(**3**). Amesema Mtume Mtukufu s.a.w.w kabla ya kudhihiri kwa MahdiError: Reference source not found a.s. makafiri watadhibiti mito mitano mashuhuri duniani. (1). Saihun,(2). Jaihun (3). Tigiris, (4). Furati, (5). Mto Nile

(**4**). Imam Ali a.s. amebashiri kudidimia na kuanguka kwa utawala wa Bani Hashim kabla ya kuja kwa Imam MahdiError: Reference source not found a.s.

(**5**). Imam Ali a. s amesema: “Zipo dalili kumi za kuja kabla ya kudhihiri kwa Imam MahdiError: Reference source not found a.s.
1. Kuchomwa motoError: Reference source not found kwa benderaError: Reference source not found katika mitaa ya Kufa

2. Error: Reference source not foundMisikitiError: Reference source not found itakuwa haitumiki

3. Njia ziendazo HijjaError: Reference source not found zitafungwa

4. baadhi ya sehemu zitadidimia ardhini

5. Kutatokezea mitetemeko mikali sana katika ardhi katika baadhi ya sehemu.

6. Watu watatoka majumbani mwao katika hali ya mivurugano

7. kutaonekana nyotaError: Reference source not found yenye mkia wa ajabu kabisa.

8. kutaonekana vitu vya ajabu mbinguni

9. kutakuwa na mauaji ya umwagaji damuError: Reference source not found

10. Unyang'anyi na wizi vitakuwa ni vitu vya kawaida. "

## Muda Wa Binadamu Juu Ya Ardhi

Abdullah ibn Umar ameripotiwa akisema: “Mwanadamu ataishi juu ya ardhi hii miaka mia moja sabini baada ya kuchomoza jua kutoka Magharibi.

## Kushirikishwa Kwa Wanawake

Imerekodiwa katika *Raudhatul – Kafi* kuwa mwanamke atapanda *mimbarError: Reference source not found* na kuwahutubia watu. Kutakuwa na wanawakeError: Reference source not found watawala na magavana na wabunge. Wanawake watashirikiana bega kwa bega pamoja na waume zao katika kazi zao. Wao watawapanda farasi na kuendesha magari n.k. Wanawake wataanzisha taasisi zao na vilabu vyao. Wanawake wataanza kutengeneza nywele zao ambazo zitakuwa sawa sawa na nundu za ngamia. Mambo yote haya yatatokea katika zama za mwisho wa dunia.

## Mzozo Wa Kuandama Kwa Mwezi

Watu watakuwa wameikhtilafiana mno juu ya swala la kuandama kwa mwezi . Wao hawatakuwa

wakifunga siku ya kwanza ya *Ramadhani* wakati ambapo siku ya *Iddi* watakuwa katika hali ya saum. Hadithi hii imetolewa katika *Biharul Anwaar.* 2

## Ala Za Muziki

Ala za muziki zitapatikana huko *MakkahError: Reference source not found* na MadinaError: Reference source not found.

## Watu Matajiri

Watu matajiri watakwenda HijjaError: Reference source not found kwa matembezi na watu wa daraja la kati watakwenda kwa ajili ya biashara na masikini watakwenda kujionyesha kuwa wao pia wanakwenda Hijja kuwa nao wanao uwezo. (*Biharul Anwaar* ).

## Ghuba Ya Aqaba

Katika kitabu cha *Ilzaam-un-Nasib* imeandikwa kuwa ardhi ya *Aqaba* itageuka kuwa nyekundu kwa sababu ya damuError: Reference source not found ambayo itamwagika kwa sababu ya vita vikali vitakavyokuwa vikiendelea hapo.

## Kuhusu Oman

Msemo huu ufuatao wa Imam Ali a. s umetolewa kutoka hutuba iitwayo *Bayyinah* amesema: "ninawasikitikia watu wa OmanError: Reference source not found kwani wao watazingirwa pande zote, waume wao watauawa na wake zao watachukuliwa mateka. "

## Kuhusu Teheran

Imam Jaafer Sadiq a.s. amesema: “Watu wa Ray (Teheran) watauawa katika mamilioni wakati huo kitovu cha elimu ya dini kitakuwa ni Qum na haya yatatokea kipindi kifupi kabla ya kudhihiri Imam MahdiError: Reference source not found a.s.

## Mafuriko, Nyoka na Nzige

Imeandikwa katika kitabu cha *Nur-ul-Anwaar* kwamba makundi makubwa makubwa ya nzigeError: Reference source not found ni dalili mojawapo ya kudhihiri kwa Imam. (imetokezea hivyo katika mwaka wa 1254 A. H. katika *Bara la Arabia*; 1268 A.H. katika IranError: Reference source not found na nchi za Sudan na Somalia tumesikia kuwa mambo haya yakitokea ). Vile vile miongoni mwa dalili za kudhihiri kwa Imam MahdiError: Reference source not found a.s. ni mafuriko, nyoka katika maji. Mambo haya ni ya kawaida siku hizi kusikia kuhusu mafuriko.

## Dalili za Ajabu na Kushangaza Mno

Mtume Mtukufu s.a.w.w alimwambia Jabir "Maisha yako yatakuwa mema na wewe utainuliwa siku ya QayamaError: Reference source not found ukiwa umeongoka. Lakini ole wa wakati ule, wakati ambapo Ukristo utakuwa na nguvu duniani na wakati ambapo ng'ombe dume watakapoanza kuongea. Zama hizo vitu vya ajabu vitaanza kutokezea. Kutakuwa na motoError: Reference source not found kila mahala (vita). Bendera ya utawala wa Othman utakuwa katika Bonde Jeusi. BasraError: Reference source not found itakumbwa na misukosuko. Baadhi ya watu watawakalia watu wengine na kuwanyanyasa. Majeshi yatatembea kati ya Taliqan, Shuyb ibn Saleh Tamim atakubaliwa. Katika Khuzistan, watu watakula viapo vya kumtii Sayyid Musawi. Bendera ya Wa-Qurdi shupavu itabuniwa. (Hadith hii ni ndefu mno isipokuwa tumechagua yale yaliyokuwa yakihusiana na somo letu. )

## Ubashiri Wa Baada Ya Vita Vya Naharwan

Baada ya Imam Ali a.s. kutokea vita vya Naharwan, alisema: "Ni jambo la kustaajabisha mno, kwa matukio yatakayotokea baina ya Jamadiul Aakhir na mwezi wa Rajab. Hakutakuwa na maelewano yoyote popote pale. Mapanga yatavuma na sauti baada ya sauti itasikika. "

## Hadith Mufadhdhal

Mufadhadhl ibn Omar alimuuliza Imam Jaafer Sadiq a.s. : “Ewe mola wangu, *Zuura* ni sehemu ipi?"

Imam a.s. alimjibu: “Hiyo ni BaghdadError: Reference source not found ambayo itakuwa ni kitovu cha adhabu na maangamizo ya Allah swt. Ole! sehemu hiyo kutachomoza kwa benderaError: Reference source not found za rangi ya njano na hapo bendera za kutoka nchi mbalimbali zitakusanyika. Adhabu za Allah swt zitateremshwa nchini humo. Matukio yasiyojulikana au yasiyopangwa au yasiyosikika au yasiyoonwa kabla ya hapo yatatokea huko Baghdad. Kutakuwa na hujuma za mapanga na hujuma hizo zitaongezeka mno. Mji huo utaongezeka kwa idadi ya watu na vile vile utakuwa ukiteketezwa, hali hiyo itakuwa ikitokezea kila mara lakini kufikia kipindi cha mwisho, kutakuwa na matendo maovu mengi sana kiasi cha kuwa mustahiki wa adhabu za Allah swt. Michafuko itakuwa imekithiri hadi hapo Hasan mtu kutoka Kazwin na Dailam atapokuja pamoja na jeshi lake juu ya mafarasi weupe. Mkuu wa kikosi chake atakuwa mtu wa Tamin ajulikanae kwa jina la Shuayb ibn Saleh. Wao watamkabili mkandamizaji na kutuliza motoError: Reference source not found wa michafuko. Baada ya hapo wataondoka kuelekea mji wa KufaError: Reference source not found.

## Wakati Maalum

Imeandikwa katika kitabu cha *Kamalud-din* kuwa Husein ibn Khalid alimwuliza Imam Ridha a.s. "Ewe Mola wangu ! Je wakati maalum ni lini. "

Imam alimjibu: "Wakati maalum ni wakati ule wa kudhihiri kwa Imam MahdiError: Reference source not found a.s.” Khalid aliuliza: "Je huyo Mahdi katika ahadi zenu ni nani?"

Imam alimjibu: “Yeye atakuwa ni wa nne katika kizazi changu, Allah swt ataondoa dhuluma na ukandamizaji duniani kote kwa kupitia huyu MahdiError: Reference source not found a.s. Kwa kuwa kipindi chake cha kuwa mafichoni (*ghaibat*) utakuwa ni muda mrefu hivyo watu wataingiwa shaka na wasi wasi na watu watakuwa na shaka iwapo amezaliwa au bado hajazaliwa.

Kabla ya kuja kwa Imam MahdiError: Reference source not found a.s. kutasikika sauti kubwa duniani kote kutoka mbinguni. Habari hiyo itawajulisha watu kuwa mwokozi wetu ameishafika karibu na Al-KaabaError: Reference source not found. Kudhihiri kwake kutaleta nuru duniani kote. Jina la baba yake ni Hasan. Yeye atakuwa ni *Qaim -bil- Haq* na *Al-Muntadhar*.

Mwenye kuripoti anauliza: "Je kwa nini majina yake yawe hayo?"

Imam alimjibu: “Watu wengi wenye kuamini katika Uimam labda watakuwa wameishageuka makafiri. Yeye ni yule anayengojewa, kwa sababu ya muda mrefu wa yeye kubakia mafichoni, katika kipindi hicho watu wengi wataanza kubishana na wataleta mzaha kwa swala zima hili, ni wachache tu walio waumini watakaosubiri tukio hili la Imam MahdiError: Reference source not found a.s. kwa wale watakaofanya haraka (kwa sababu watatokezea wengi ni waongo). Basi hao watakuwa wamepotea na wale Waislamu halisi wataokoka.

## Madondoo Ya Kudhihiri Imam : Kitab Al- Irshad

Kutoka dalili na mabashiri ya kudhihiri kwa Imam MahdiError: Reference source not found a.s. hapa kuna madondoo machache ambayo yamechambuliwa
1. Uasi wa *SufianiError: Reference source not found*,

2. kuuawa kwa Hasan

3. Ikhitilafu baina ya Bani Abbas kwa matakwa ya dunia

4. Kupatwa kwa jua katika mwezi wa Ramadhani, ikifuatiwa na kupatwa kwa mwezi mwishoni mwa mwezi huo wa Ramadhani

5. Beda (mahala baina ya *MakkahError: Reference source not found* na MadinaError: Reference source not found) itadidimia ardhini,

6. Ardhi katika upande wa Mashariki na upande wa Magharibi zitadidimia

7. Jua wakati wa asubuhi litaonekana liko papo hapo bila kutembea hadi wakati wa mchana na baadaye litachomoza kutoka Magharibi.

8. Mcha Mungu atauawa nyuma ya msikiti wa KufaError: Reference source not found pamoja na watu sabini wengine

9. Mtu mwema kutoka ukoo wa Bani Hashim atachinjwa baina ya *Rukn* na *Makam* huko *MakkahError: Reference source not foundError: Reference source not found*.

10. Kuta za Msikiti wa Kufa zitaporomoka

11. Bendera nyeusi zitatokezea huko Khorasan

12. Mtu kutoka YemenError: Reference source not found ataongoza uasi.

13. Mtu atakayetokea nchi za *Maghreb* ataonekana huko MisriError: Reference source not found na ambapo atapata mamlaka makubwa

14. WarusiError: Reference source not found watafika *Bara la Arabia*

15. WazunguError: Reference source not found watafika PalestinaError: Reference source not found.

16. Upande wa Mashariki kutaonekana kwa nyotaError: Reference source not found yenye mkia. Mwanga wake utaonekana kama ule wa mwezi na ncha zake zote zitakuwa moja (zitaungana).

17. Kutaonekana uwekundu mkubwa sana mbinguni.

18. Kutazuka motoError: Reference source not found mkubwa sana katika Mashariki ya kati ambayo itadumu kwa muda wa siku tatu hadi saba.

19. Wale wasio Waarabu watawafukuza Waarabu kutoka ardhi zao

20. Utawala wa kifalme utakwisha nchini Iran

21. Wamisri watamuua kiongozi wao

22. Bendera tatu zitakusanyika Syria

23. Kutazuka mizozo mikubwa na Syria itateketezwa

24. Bendera za Waarabu na Bani Qais zitatoka Misri

25. Bendera ya Banu Kinda itapepea Khorasan

26. Jeshi kubwa sana litapita Hira

27. mabango meusi yatafika kutokezea Mashariki

28. Maji ya mito ya Furat yatafurika katika mitaa ya Kufa

29. Kutatokezea watu sitini watakaodai kuwa wao ni Mitume.

30. Sayyid kumi na wawili watadai kuwa wao ni Imamu Mahdi

31. Mtu mwenye heshima kubwa kutoka Bani Abbas atachomwa moto hai karibu na Khankin

32. Kutajengwa na daraja katika BaghdadError: Reference source not found katika sehemu za Kharah

33. Kutakuwa na tufani ya upepo mkali katika Baghdad wakati wa asubuhi na kutafuatiwa na kupasuka kwa ardhi ambamo baadhi ya sehemu itadidimia ardhini

34. Mauti, vifoError: Reference source not found na maangamizo yatakithiri huko IraqError: Reference source not found kiasi kwamba watu watakuwa kama wamewehuka

35. vikundi vitapigana mno huko Iran

36. Sura za jumuia zitachafuliwa

37. Watumwa wataanza kutawala nchi za Mabwana wao

38. Sura kama ya binadamu itaonekana karibu na jua

39. Makaburi yatafumuliwa na

40. waliokufa watapewa uhai

41. Kutakuwa na mvuaError: Reference source not found itakayonyesha kwa mfululizo wa siku ishirini na nne ambayo itahuisha ardhi iliyokuwa imekufa.

Kwa hakika wakati huo ndio utakuwa wakati wa kudhihiri kwa Imam Mahdi a.s.

Miongoni mwa dalili na bashara za hapo juu kuna mengineyo yenye masharti. Allah swt tu anaelewa kitakachotokea na lini.

## Mafafanuzi ya Dalili na Bashara kwa Mukhtasari

Vitabu vingi vimeandikwa juu ya bashara na dalili za kipindi kabla ya kudhihiri kwa Imam MahdiError: Reference source not found a.s. kwa hakika swala hili lipo kwa mapana sana kiasi kwamba ni vigumu mno kukusanya kwenye kitabu kama hiki. Hata hivyo kumefanywa juhudi kubwa sana ya kuweza kukusanya mabashiri haya kwa kiasi ilivyowezekana. Tumejaribu kuona kuwa mengi yametokezea na mengi bado yatatokezea. Wakati unakwenda ukiiva kwa ajili ya matukio mengine kutokezea, na mengine yapo yanatokezea lakini habari bado hatujazipata. Hapa chini tumejaribu kutoa baadhi ya maelezo yetu ambayo hatuwezi kujidai kuwa sisi ni mabingwa wa mambo haya, anayejua zaidi ni Allah swt peke yake.

Inaonekana kuwa sura ya Islam itabadilika sana siku za mbeleni. Mashauriano yataonekana ni mambo ya upweke. Kutatokea mabadiliko katika maisha ya jamii na ya kijumuia na ya kiutamaduni,tamaduni za binadamu zitachafuliwa mno. Hukumu za Allah swt zitapuuzwa na hazitatekelezwa. Watu watawakimbilia wale wasio mtii Allah swt, hivyo dunia nzima itajawa kwa vitisho na ukandamizwaji. Haki na usawa utakuwa umetokomezwa kabisa. Maasi na madhambi yatakuwa yamekithiri kila mahala.

Kwa yote yaliyoandikwa hapo juu inamaanisha waziwazi kuwa ulimwengu umejiandaa kwa ajili ya adhabu na ghadhabu za Allah swt na wa hakika kama tutatenda kinyume na maamrisho ya Allah swt basi hivyo tukae tayari kwa ajili ya adhabu zake.

Mwanzoni mwake kutatokezea kwa michafuko huko Mashariki ya Kati ambayo yataenea dunia nzima hapo baadaye. Kutatokezea maajabu mbinguni na kuonekana kwa nyotaError: Reference source not found yenye mkia inayong'aa huko mbinguni.

WarusiError: Reference source not found wataanza kuingilia kati mambo ya Mashariki ya Kati. WazunguError: Reference source not found watajiingiza huko PalestinaError: Reference source not found na kuleta uchafuzi. Na hivyo kutaanza kwa vita ambavyo vitaenea duniani kote. Labda itawezekana silaha za kinyukilia zikatumika huko na zikasababisha mitetemeko ya ardhi, kudidimia kwa ardhi na kuteketezwa kwa watu. Baadhi ya sehemu zitateketezwa kabisa. Nchi za Kiisilamu zitaathirika sana kwa hayo. Vita hivyo vya huku na huko mwisho vitakuja kuwa vya dunia nzima. MisriError: Reference source not found itachafuliwa kabisa kabisa. BaghdadError: Reference source not found na BasraError: Reference source not found vitateketezwa kabisa, miale ya mioto itatokezea *Bara la Arabia.* Kutalipuka motoError: Reference source not found mkali sana katika sehemu za machimbo ya mafuta huko Aden.

Katika vita hivi vya dunia, kutatumiwa silaha mbaya kabisa zenye kuleta maangamizo na maafa makubwa kabisa. Anga zetu zitakuwa zimejaa kwa gesi ya sumu kali. Kujiingiza kwa WachinaError: Reference source not found katika vita hivi kunamaanisha hali kuchafuka kabisa. Takriban theluthi moja ya dunia nzima watauawa katika vita hivi.

Baada ya kumalizika kwa vita hivi itafuatia hali ya kuangamiza kabisa. Kutatokezea magonjwa ya kuambukizwa, kutatokezea balaaError: Reference source not found za kila aina ambazo zitaharibu maisha ya watu na watu watakufa wengi mno. Ukame utawamaliza watu wengi sana kiasi cha theluthi moja ya wakazi wa dunia nzima wataweza kuponea chupuchupu maafaError: Reference source not found haya.

Mwanadamu ameishafika mwezini, Imam Jaafer Sadiq a.s. amesema kuwa uso wa mwanadamu utaonekana mwezini na mkono wake utaonekana mbinguni yaani mwanadamu ataweza kuzishinda anga za juu. Binadamu pamoja na kuwa na maendeleo haya ya kisayansi lakini kwa kutokuwa na umoja, upendo na undugu wataimaliza dunia. Utumiaji wa silaha za kisasa na za hatari kabisa zitabadilisha hali ya hewa ya ulimwenguni na taratibu za jua zitaathirika sana, hasa dunia yetu hii. Kwa

hali hii ama jua litaonekana limebaki pale pale ama dunia yetu hii itaacha kuzunguka kuanzia asubuhi hadi mchana. Kwa hivyo kutatokezea kupatwa kwa jua na mwezi kwa mwezi mmoja jambo ambalo kihesabati haiyumkiniki kwa sasa.

